# Nipashe

Ijumaa Aprili 17, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580208

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Aliyemdanganya waziri kuwa ana virusi vya corona mbaroni

UKURASA 3



BUFE

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ujue umoja wa walemavu wenye mashine ya kusaga, shida palepale

BIASHARA

Maswali mazito Ushetu, ukoje utata Rea kuwaweka kando umeme wao?

WAZIRI, RAS, DIWANI WAJIBU....

UKURASA 11

# Bei ya sukari yatisha

**YAADIMIKA** sokoni, serikali yaagiza tani 20,000...*Endelea ukurasa 2*




Mfanyabiashara Rostam Aziz (kushoto), akipita kwenye mashine maalumu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, baada ya kukabidhi mashine hizo na vitakasa mikono vyenye thamani zaidi ya Sh. milioni 600 kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (hayupo pichani), jijini Dar es Salaam jana. Habari Uk. 7. PICHA: **MPIGAPICHA WETU**

## BAA LA CORONA



Mambo ya kuzingatia katika kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona ni pamoja na kutovuta sigara, kutokuvaa zaidi ya barakoa moja kwa wakati mmoja na kutumia kiuavijasumu (antibiotics). WHO

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

# Wagonjwa wa corona wafikia 94

**WATAKAOKWENDA** MOI kuvaa barakoa...*Endelea ukurasa 2,3*

## UKUTA WAUA WANNE FAMILIA

UKURASA 3


Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** LIGI KUU BARA BADO SHAKANI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Watuhumiwa wa biashara ya dawa za kulevya, wakiwa chini ya ulinzi baada ya kukamatwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini, wakiwa na zaidi ya kilogramu 270 za Heroin katika eneo la Mbezi Kibanda cha Mkaa, jijini Dar es Salaam. Kutoka kushoto ni raia wa Nigeria, Kanayo David Chukwu (39) na raia wawili wa Tanzania Isso Romward Lupembe (49) na Amon Mbele(38). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bei ya sukari yatisha

**Na Waandishi Wetu**

BEI ya sukari katika maeneo mbalimbali nchini, imezidi kupaa huku ikiadimika kwenye maduka ya rejareja na jumla.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe katika maeneo mikoa mbalimbali ulibaini kwa sasa kilo moja ya sukari inauzwa kati ya Sh. 2,800 hadi 4,500 gharama inayowafanya watu kushindwa kuimudu.

Jijini Dar es Salaam kilo moja inauzwa kati ya Sh. 2,800 hadi 4,500, huku ikiadimika katika maduka ya jumla kwa wauzaji wa rejareja.

Mmoja wa wauzaji wa rejareja eneo la Salasala, Zainab Ismail, alisema kabla ya mabadiliko, alinunua mfuko wa kilo 50 kwa Sh. 55,000 ikiwa ni wastani wa kilo moja kwa Sh. 2,200 na kuuza dukani kwake kwa Sh. 2,600, lakini kwa sasa ananunua mfuko huo kwa Sh. 70,000 ikiwa ni sawa na Sh. 2,800 kwa kilo moja na kulazimika kuuza Sh. 3,200.

Mnunuzi mwingine aliyekwenda kwenye maduka ya jumla eneo la Manzese, alikosa bidhaa hiyo na kwenye baadhi ya maduka ilipanda na kufikia Sh. 80,000 hadi 100,000 kwa mfuko wa kilo 50.

"Sasa nikinunua kwa bei ya jumla Sh. 80,000 maana yake nimenunua kilo moja kwa Sh. 3,200 nikauze Sh. 3,800 ili nipate faida ya Sh. 500 kwa kila kilo, nikinunua kwa Sh. 100,000 maana yake kilo ni Sh. 4,000 nami itanibidi niuze kwa Sh. 4,500," alisema.

Waliiomba serikali kuingilia kati kwa kuwa wafanyabiashara wakubwa wamehifadhi sukari kwenye maghala na kuwafanya wananchi wateseke kwa bidhaa hiyo kuadimika.

Mkoani Iringa bidhaa hiyo inauzwa Sh. 3,000 kwa kilo, huku mkoani Shinyanga ni kati ya Sh. 3,000 hadi 3,200.

Mkoani Arusha ni kuanzia Sh. 3,600 hadi 4,000, huku mkoani Katavi ikiuzwa kwa Sh. 3,000 na Songwe ikianzia Sh. 2,700 hadi 3,500.

Kwa upande wa visiwani Zanzibar imeonekana kuwa na nafuu kwa kuuzwa kwa Sh. 1,800 kwa kilo moja.

"Maisha yanazidi kuwa magumu kwa sasa na janga hili la corona bidhaa kama hii inapopanda bei inaharibu bajeti yetu kidogo tuliyonayo," alisema Asha Juma mkazi wa Tegeta.

Mkoani Morogoro bidhaa hiyo inauzwa kati ya Sh. 3,500 hadi 4,000 kwa maeneo tofauti.

Viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo nchini ni TPC, Mtibwa, Kagera na Kilombero.

Kufuatia hali hiyo, serikali imesema itawachukulia hatua kali za kisheria wafanyabiashara watakaobainika kuficha sukari katika maghala yao kwa lengo la kupandisha bei wakati huu wa janga la corona.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alisema hayo wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jiji Dodoma, kuhusu ya malalamiko ya kupanda kwa bei ya sukari nchini.

Waziri Bashungwa alisema, hivi sasa serikali imeunda tume itakayokuwa na jukumu la kupita katika maeneo mbalimbali na kukagua maghala ya wafanyabiashara ambayo yanatumika kuficha bidhaa hiyo muhimu ya sukari.

Alisema tume hiyo itahusisha wataalamu wa wizara na kujumuisha maofisa biashara wa mikoa yote nchini ambao watafanya kazi kwa pamoja kukagua maeneo.

"Nawatahadharisha wafanyabiashara wote walioficha sukari kwenye maghala yao kwa lengo la kupandisha bei na kujipatia faida, kuacha tabia hiyo mara moja, watakao bainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao," alisema Bashungwa.

Alisema hivi sasa serikali inafanya jitihada za kuongeza uzalishaji wa sukari na kuwa wafanyabiashara watakaobainika kuhodhi sukari watachukuliwa hatua kali.

Pia Bashunga, alisema serikali imeagiza zaidi ya tani 20,000 za sukari kutoka nje ya nchi ikiwa ni tahadhari ya kuwa na akiba ya kutosha ya bidhaa hiyo katika kipindi hiki cha janga la maambukizi ya virusi vya corona na kuelekea mwezi mtukufu wa mfungo wa Ramadhani.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakazi jiji la Dodoma wamesema bei ya sukari katika maduka ya rejareja imepanda kutoka Sh. 2,600 kwa kilo hadi Sh. 3,500 na kuiomba serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha inadhibiti mfumuko wa bei ya bidhaa hiyo muhimu.

Waziri Saleh, mkazi wa Mailimbili jijini Dodoma, alisema serikali inatakiwa kuchukua hatua za haraka kudhibiti mfumuko huo wa bei ili kuwasaidia wananchi katika kipindi hiki cha janga la corona.

Vilevile, aliitaka serikali kutoa bei elekezi nchi nzima kwa madai wafanyabiashara kuwa na tabia ya kusingizia corona kama sababu ya kupanda bei kwa bidhaa nyingi.

"Kama serikali haitakuwa makini, basi kila mfanyabiashara atasingizia corona kupandisha bei kama anavyotaka, ili kuepusha hili serikali ikemee wafanyabiashara wote wenye tabia hii haraka," alisema.

Naye mmoja wa wafanyabiashara ya kupika vitumbua, Sauda Swalehe, alisema kutokana na kupanda bei kwa sukari wanafanya biashara kwa hasara.

Alisema serikali iwaangalie wajasiriamali wadogo kama yeye kwa kuwa hali zao hivi sasa ni ngumu, kutokana na janga la corona biashara zao zimeyumba hivyo mzigo wa kupanda bei kwa sukari unaendelea kuwaumiza.

***Imeandikwa na Salome Kitomari (Dar) na Paul Mabeja (Dodoma)**

# Wagonjwa wa corona wafikia 94

**Na Romana Mallya**

WAGONJWA wengine sita wanaougua ugonjwa wa corona wameongezeka visiwani Zanzibar na kufanya idadi kwa Tanzania kufikia 94.

Waziri wa Afya, Zanzibar, Hamad Rashid Mohammed, katika taarifa yake aliyoitoa jana, alisema ongezeko la watu hao sita visiwani huko kunafanya mpaka sasa idadi ya wanaougua kufikia 24.

"Waliopatikana ni mkazi wa Kibweni (30), mkazi wa Magogoni (27), mkazi wa Kwarara (28), mkazi wa Kilimahewa Juu (58), mkazi wa Amani (23) na mkazi wa Kidoti (55)," alisema.

Waziri Mohammed alisema wagonjwa wote hawana historia ya kusafiri nje ya nchi siku za hivi karibuni na kwa sasa wamelazwa katika vituo maalum kwa ajili ya kuendelea na matibabu.

"Serikali kupitia wizara ya afya, inaendelea kuwasisitizia wananchi kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa huu zinazotolewa kila mara," alisema.

Pia waziri huyo aliwataka wananchi wenye dalili za homa kali, kukohoa na kupiga chafya kujitokeza katika vituo vya afya au kupiga simu namba 190.

Waziri Mohammed aliwataka wananchi wanaopatwa na misiba wachukue tahadhari ya namna ya kuwashughulikia, kuwakafini na kuwazika maiti.

"Tunawashauri ni vyema wakashirikiana na wataalamu wa afya kupata miongozo stahili," alisema.

**ELIMU MAALUM DAR**

Wakati huo huo, serikali jana ilizindua mpango maalum wa kutoa elimu ya afya kwa umma mkoani Dar es Salaam, wenye lengo la kukata mnyororo wa maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo jana jijini humo, wakati akizundua mpango huo wa siku 20 ambao utaongozwa na vikundi vya kijamii kwa kushirikiana na Red Cross chini ya wizara yake.

"Lengo la kuzindua mpango huu ni kukata mnyororo wa maambukizi ya ugonjwa wa corona kati ya mtu na mtu kwa kutumia vikundi vya kijamii ambavyo vitaelimisha na kutoa taarifa sahihi kwa jamii kuhusu ugonjwa wa Corona.

Alisema vikundi hivyo vya kijamii vitashirikiana na wizara, Red Cross na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia watoto na wanawake katika mataifa yanayoendelea (UNICEF) kutoa elimu ya afya kwa umma.

Alisema katika mpango huo jumla ya magari 18 yatatumika kwa siku 20 na yatakwenda katika maeneo ya masoko, stendi za mabasi na maeneo mengine yenye mikusanyiko ya watu kutoa elimu.

"Siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili, vikundi vya kijamii vitakwenda katika maeneo ya nyumba za ibada kwa ajili ya kuongeza nguvu ya kutoa elimu ya afya.

"Niwatoe hofu Watanzania, tutashinda hii vita endapo kila mmoja katika Jamii atazingatia maelekezo ya Wataalamu wa Afya."

Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Afya kwa Umma wa Wizara ya Afya, Dk. Ammaberg Kasangala, alisema atahakikisha mpango huo unatekelezwa.

HABARI KITAIFA

# Aliyemdanganya waziri kuwa ana virusi vya corona mbaroni

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MUSSA Kisinza (25), mkazi wa Kijiji cha Mwakitolyo, wilaya ya Shinyanga, anashikiliwa na Jeshi la Polisi, kwa tuhuma za kumpigia simu na kumdanganya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, kuwa ana virusi vya corona.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alisema mtu huyo baada ya kupiga simu kwa waziri na kumueleza kuwa amepata maambukizi ya corona, timu ya madaktari ilikwenda eneo hilo, lakini walipofika simu yake ilizimwa. Alisema baada ya mtu huyo kuzima simu yake aliyotumia kumpigia waziri, timu ya madaktari walikosa mawasiliano yake, hivyo kulazimika kurudi.

"Tunamshikilia Mussa Kisinza kwa kutoa taarifa ya uongo kwa kumpigia simu na kumdanganya waziri wa afya kuwa ana ugonjwa wa Covid 19 unaosababishwa na virusi vya corona, wakaia haumwi," alisema Magiligimba.

Kwa mujibu wa Magiligimba, baada ya mtu huyo kuzima simu na kuleta taharuki, kikosi kazi cha askari wa makosa ya kimtandao, juzi walifika eneo hilo na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa huyo, baada ya kumkuta akiendelea na shughuli zake za uchimbaji wa dhahabu.

Alisema walipomkamata wakiwa na timu ya madaktari, walimfikisha kwenye zahanati ya kijiji hicho, na walipomfanyia vipimo vya awali vya magonjwa nyemelezi yanayoashiria kuwa na ugonjwa wa virusi vya Corona, aligundulika hana ugonjwa wowote.

Magiligimba aliwataka wananchi, kuacha masihara juu ya ugonjwa wa Covid 19, na kubainisha kuwa mtu yeyote atakayetoa taarifa za uongo juu ya ugonjwa huo, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Al–Hekma, Nurdeen Kishk (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kufuta mashindano ya Qur'an ya Afrika yaliyotarajiwa kuanza mwezi tukufu wa Ramadhan, kutokana na tahadhari ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona. Wengine ni wajumbe wa Kamati ya Maandalizi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watakaokwenda MOI kuanza kuvaa barakoa

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa (MOI), imewataka ndugu wote wanaokwenda kuona wagonjwa na wadau wengine watakaofika katika taasisi hiyo kuanzia leo wavae barakoa (mask).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na kitengo cha uhusiano Moi kupitia Ofisa Habari wake, Patrick Mvungi, huo ni mkakati wa taasisi wa kuhakikisha ndugu wa wagonjwa na wadau wanakuwa salama dhidi ya virusi vya corona.

"Ni lazima kusafisha mikono kwa vitakasa mikono kila wanapoingia na kutoka ndani ya taasisi hii na kupimwa joto la mwili," alisema.

Machi 16, Tanzania ilithibitisha kisa cha kwanza cha mgonjwa wa corona, Isabella Mwampamba (46), aliyetokea nchini Ubelgiji na kutua katika Uwanja wa Ndege wa KIA mkoani Kilimanjaro.

Machi 31, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, ilitangaza kifo cha kwanza cha Mtanzania mwenye umri wa miaka 49 kufariki kwa Corona ambaye pia alikuwa akisumbuliwa na maradhi mengine.

Hadi sasa, waliofariki dunia kwa ugonjwa huo ni watu wanne miongoni mwao mwanawake ni mmoja na waathirika waliopo hadi sasa ni watu 94 kutoka Tanzania Bara na visiwani Zanzibar.

Duniani kwa mujibu wa kituo cha Chuo Kikuu cha Johns Hopkins nchini Marekani, walioambukizwa hadi sasa ni watu 2,072,228 huku kukiwa na vifo 137,666 wakati nchi na maeneo ya utawala yenye maambukizi ni 185.

# Wanne familia moja wafa kwa kuangukiwa na ukuta

**Na Ndalike Sonda**

KAWATOTO wanne wa familia moja, wamekufa baada ya kuangukiwa na ukuta wa nyumba wakiwa wamelala usiku wa kuamkia jana katika kijiji cha Chalya, Kata ya Nyandekwa Halmashauri ya mji wa Kahama, mkoani Shinyanga.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, akizungumza na Nipashe, aliwataja watoto waliokufa kuwa ni Emmanuel Yona (2), Monica Yona (5), Tatu Yona (10) na Lusina Yona (13) huku mama yao Sarah Bundala akipata majeraha kidogo, kutibiwa na kuruhusiwa kurejea nyumbani.

Alisema chanzo cha awali cha nyumba hiyo kuanguka ni kutokana na udhaifu wa kuta zilizojengwa kwa tofali za tope.

Alisema baada ya Kamati ya Usalama ya Wilaya ya Kahama kufika eneo hilo, ilitoa maelekezo ya serikali na kuagiza miili hiyo izikwe na gharama za majeneza zimetolewa na Serikali ya Wilaya ya Kahama, na kwamba baada ya mazishi ni vyema watu wakasambaa ili kuendelea kuchukua tahadhari ya virusi vya corona.

Alisema wameelekeza wananchi wa kijiji hicho wajaribu kuwahifadhi kwa muda wazazi wa watoto hao ambao kwa sasa hawana nyumba na uongozi wa kijiji na kata uangalie namna ya kuwajengea nyumba nyingine ya muda huku akiwataka wananchi kuchukua tahadhari ya mvua inazoendelea kunyesha pamoja na kujenga makazi imara ya kudumu.

Baadhi ya mashuhuda waliofika katika tukio hilo, walisema tukio hilo limewashtua na wataendelea kuchukua tahadhari. Jeshi la Polisi wilayani Kahama lilifika eneo la tukio likiwa na mkuu wa wilaya ya Kahama na kuruhusu shughuli za mazishi ziendelee kwa kuzingatia tahadhari ya janga la virusi vya corona.


bgtl BEST GROUP (T) LIMITED
Debts Collectors, Auctioneer, Commission Agent, Court Broker & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK (TZ) LTD** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo huo kwa **MNADA WA HADHARA.**Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | JINA LA MMILIKI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO |
|---|---|---|---|
| 1. | ELIPOKEA ELISANTE KWAYU | ELIPOKEA ELISANTE KWAYU | Nyumba yenye leseni ya makazi ardhi na.ILA/KWN/YMB20/53 Iliyopo kata ya Kiwalani mtaa wa Yombo Manispaa ya Ilala |
| 2 | SERERYA JOSWAN RANGE | SERERYA JOSWANI RANGE | Nyumba yenye leseni ya makazi ardhi na.TMK/MBGL/KZG9/347 Iliyopo Kata ya Mbagala Mtaa wa Kizinga manispaa yaTemeke |

**MASHART YA MNADA**

1.Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2.Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3.Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4.Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road.
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537

AU

Mkurugezi Mtendaji
Equity Bank (Tz)Limited
Head Office,
Ohio street-Golden Jubilee Towers,
P.O. BOX 110183,
DAR ES SALAAM
MOBILE; + 255 768985500
Email: info@equitybank.co.ke

157038

# Uboreshaji daftari waanza Mwanza

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WANANCHI mkoani Mwanza wametakiwa kutumia fursa ya uboreshwaji wa daftari la kudumu la wapigakura kurekebisha taarifa zao ili waweze kupata sifa za kupiga kura kwenye uchanguzi mkuu wa mwaka huu.

Akizungumza wakati akipokea msaada wa vifaa vya kujikinga na virusi vya corona (Covid-19) kutoka kwa wadau mbalimbali mkoani humo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema uboreshaji huo utaanza leo hadi Aprili 19 na kuhusisha wilaya zote saba kwa siku tatu.

"Dhima la zoezi ni kuandikisha raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 na wale ambao watatimiza umri huo siku ya uchaguzi, kurekebisha taarifa za wapigakura waliohama, kuondoa wapigakura waliopoteza sifa na kutoa kadi mpya kwa wapigakura waliopoteza au kadi zao kuharibika," alisema Mongella.

Aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kwa kuwa kila Mtanzania ana haki ya kushiriki, pia ushirikishwaji wa vyama vya siasa katika maeneo mengine ya mchakato wa uchaguzi, vyama vinaruhusiwa kuweka mawakala wao katika vituo vya kuandikisha wakati wa uboreshaji wa daftali hilo.

Alitoa tahadhari ya ugonjwa wa Covid-19 kuwa utazingatiwa kikamilifu wakati wa uboreshaji huo na vituo vyote 191 vilivyopo kwenye kila kata wataweka sabuni za kusafisha mikono, maji tiririka, vitakasa mikono na spiriti za kusafishia vifaa vya uandikishaji.

Pia, alitoa shukrani kwa viongozi wa dini na kuwataka kuendelea kujizatiti kwa kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kufuata na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Wizara ya Afya ili kujikinga na kuepukana na maambukizi ya ugonjwa huo.




Mratibu wa vipindi wa EATV, Sophia Proches (kushoto), akizungumza na kiongozi wa kampeni ya Nyumba ni Choo ambayo ipo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Kaposo Mwambuli (Kulia), akiwa na Ofisa Uhusiano wa kampeni hiyo, Kemi Mutahaba, walipotembelea vyombo vya habari vya IPP, Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Kortini madai kutumia jina la Janeth Magufuli kutapeli

**Na Hellen Mwango**

WAFANYABIASHARA wawili wakazi wa jijini Dar es Salaam, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakikabiliwa na mashtaka matatu ikiwamo kuchapisha taarifa za uongo, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha zaidi ya Sh. milion 15 kutumia jina la mke wa Rais, Janet Magufuli.

Washtakiwa hao ni, mkazi wa Tegeta Wazo, Nkinda Shekalaghe (34) na mkazi wa Kitunda Magore, Masse Uledi (43).

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustina Mmbando.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mawakili wa Serikali Waandamizi, Mkunde Mshanga na Wankyo Simon.

Mshanga alidai kuwa kati ya Januari na Machi 31, mwaka huu, washtakiwa kupitia mtandao wa Facebook walichapisha taarifa kwamba 'Janet Magufuli Saccos' "Mpya mpya isome tafadhali mkopo yote ni online tuu! Na utaupata ndani ya dakika 45 tu, mikopo huanza kutolewa kuanzia laki tatu hadi milioni ishirini fuata utaratibu huu ili kupata mkopo...tuma namba za kitambulisho chako cha mpiga kura au nida na majina yako matatu kupitia namba hii 0685012921 kisha piga namba hiyo ili upatiwe namba ya mhasibu ili kuweka akiba hatimaye kupata mkopo..." Huku wakijua ni uongo.

Shtaka la pili, washtakiwa wanadaiwa kuwa kati ya Januari na Machi 31, mwaka huu, kwa pamoja walitoa taarifa za uongo na kujipatia miamala ya fedha kwa njia ya simu kutoka mahali tofauti na kujipatia Sh. 15,068,650 kutoka kwa watu tofauti.

Wankyo alidai katika shtaka la tatu, kati ya Januari na Machi 31, mwaka huu mahali tofauti nchini walitakatisha fedha hizo huku wakijua ni kosa tangulizi la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi ya Uhujumu Uchumi.

Hakimu Mmbando alisema kesi hiyo itatajwa Aprili 30, mwaka huu na washtakiwa wapelekwe mahabusu.

# PM aonya msongamano ibadani

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amekemea mikusanyiko kwenye nyumba za ibada, ikiwa ni mojawapo tahadhari ya kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19.

Akizungumza na wahabari juzi jioni kwa njia ya video akiwa ofisini kwake Dodoma, alisema ipo haja ya kuongeza nguvu ya kutoa elimu kwa wananchi wajue jinsi gani ya kujilinga na corona.

Alisema Serikali ilitoa karantini kwa shughuli za mwanzo kwa mwezi mmoja, lakini sehemu hizo zitaendelea kutoa huduma hadi hapo tamko litakapotoka kwani bado hatua za kupambana na ugonjwa huo zinaendelea.

"Pamoja na vibali tulivyotoa vya kuendesha ibada, lakini naambiwa kumekuwa na mfumo wa kuanzisha madarasa (Sunday School) ya watoto wadogo kwenye misikiti na makanisa hayo ni maeneo ambayo tuliyawekea karantini, hivyo mfumo huo usitishwe," alisema na kuongeza:

"Tuliongea na viongozi wa dini na tukaruhusu ibada tu na sio kitu kingine, na ibada hiyo iwe fupi na wakae kwa nafasi ili kuepusha msongamano," alisema.

Aidha, alisema ikiwezekana wachaguliwe watu wachache wakafanye ibada, na Serikali haitapenda kuingilia masuala ya kidini, hivyo maaskofu na mashehe walielewa jambo hilo, na kwamba ni vyema wakasaidia ili lisilete madhara makubwa.

Kwa upande wa maeneo ya masoko, maduka na 'supermarket', alisema watu waendelee kupata huduma na Serikali haikusudii kusitisha utoaji wa huduma hizo huku akiwataka wahudumu kuhakikisha wanaweka vitakasa mikono kwenye milango.

Hadi sasa Tanzania ina jumla ya visa 94 ikiwa ni 24 Zanzibar na 70 Tanzania Bara, kati yake waliofariki ni wanne, waliopona ni 11.

Duniani kwa mujibu wa kituo cha Chuo Kikuu cha Johns Hopkins nchini Marekani, walioambukizwa hadi sasa ni watu 2,072,228 huku kukiwa na vifo 137,666 wakati nchi na maeneo ya utawala yenye maambukizi ni 185.

# Akamatwa na kilo 270 za heroin

**Na Mwandishi wetu**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, jana ilikamata raia wa Nigeria, Kanayo David Chukwu (39) mkazi wa Masaki Jijini Dar es Salaam, akiwa na kilogramu 270 za heroin.

Pia, wanashikiliwa raia wawili wa Tanzania, Alistair Amon Mbele (38) ambaye ni mkutubi wa Chuo Kikuu cha Aghakan jijini Dar es Salaam, mkazi wa Mbezi Kibanda cha mkaa na Isso Lupembe (49), ambaye ni mkazi wa Mbezi Louis na Changanyikeni.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Kamishna wa Mamlaka hiyo, James Kaji, alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakifanya biashara hiyo kwa muda mrefu nchini na kwamba mamlaka imefanikiwa kukamatwa kwa watu hao kutokana na ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na nchi nyingine katika kupambana na tatizo la dawa za kulevya duniani kwa utaratibu wa kubadilishana taarifa ambazo husaidia kurahisisha ukamataji huo.

Watuhumiwa walikamatwa na dawa za kulevya aina ya heroin zinazokadiliwa kuwa na zaidi ya kilogramu 270 zilizokuwa zimehifadhiwa kwenye moja ya nyumba iliyopo Mbezi kibanda cha mkaa, jijini Dar es Salaam.

"Baada ya kupata taarifa kutoka kwa vyombo mbalimbali vya usalama ndani na nje ya nchi, tulianza kuwafuatilia toka tarehe nane na kufanikiwa kuwaweka mtegoni tangu wakiwa wanateremsha mzigo na kufanikiwa kuwakamata."

"Pia, watuhumiwa hao walikuwa wamefanya maandalizi ya kupokea mzigo huo kwa kujenga tangi la maji machafu ambalo liliwekwa chemba juu ya kuhifadhia dawa hizo na bahati mbaya mzigo uliwahi kufika kabla tangi halijakamilika, hivyo kulazimika kuzihifadhi ndani ya nyumba," alisema Kamishna Kaji.

Alitoa rai kwa wananchi kuunga mkono jitihada za serikali katika kupambana na biashara ya dawa za kulevya kwa ajili ya kuokoa maisha ya Watanzania kwa kutoa taarifa wanapoona matukio yasiyo ya kawaida kwa usalama.

"Kilo hizi ni nyingi sana zingeingia mtaani zingeathiri nguvu kazi ya vijana wetu kwa kiasi kikubwa,"alisema na kuongeza: "Ninasikitika kuona bado kuna watu wasio na utu wanaendelea kujitafutia kipato kwa njia hii haramu bila kujali. Ninatoa rai kwa Watanzania walio tayari kuwapambania watoto wao kuendelea kushirikiana na Mamlaka kuwafichua watu hawa bila woga," alifafanua.

Alisema watuhumiwa wako mikononi mwa mamlaka na watafikishwa mahakamani baada ya taratibu kukamilika ili sheria ichukue mkondo wake.

# Zungu aanika vigingi vitatu vya muungano na mazingira

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, ameanika vigingi vitatu vilivyoikabili wizara hiyo katika utekelezaji wa majukumu yake mwaka huu wa fedha. Akiwasilisha bungeni jijini hapa jana, hotuba kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Zungu alivitaja vikwazo hivyo kuwa ni pamoja na upungufu wa idadi inayostahili ya watumishi katika kusimamia shughuli za muungano na mazingira.

Zungu alikitaja kikwazo cha pili kuwa ni kukosekana kwa mfumo thabiti wa ushirikiano baina ya taasisi za serikali kuhusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Alisema kikwazo kingine ni uelewa mdogo wa jamii kuhusu uhifadhi na usimamizi wa masuala ya mazingira na uzingatiaji mdogo wa jamii kuhusu sheria, kanuni na taratibu za uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

"Katika kukabiliana na changamoto (vikwazo) hizi, ofisi ilichukua hatua kwa kuwasiliana na Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora kwa ajili ya kuongezewa rasilimali watu; kufanya vikao vya ushirikiano kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais na OR-Tamisemi kubaini aina ya mfumo utakaotumika kuimarisha ushirikiano katika kutekeleza kazi za uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

"Pia, iliendelea kutoa elimu kwa umma juu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira na umuhimu wa kuzingatia sheria na kanuni za mazingira kupitia vyombo vya habari na maadhimisho mbalimbali," alisema.

**VIPAUMBELE 2020/21**

Zungu alisema kuwa katika mwaka ujao wa fedha, wizara yake itaratibu vikao vya kamati ya pamoja ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushughulikia masuala ya muungano.

Alisema wizara hiyo pia itaratibu masuala ya kiuchumi na kijamii kwa kufuatilia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa pande mbili za muungano, kuhakikisha gawio la asilimia 4.5 ya Fedha za Misaada ya Kibajeti (GBS), faida ya Benki Kuu, Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo na PAYE linapelekwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wadau, serikali toeni elimu ya corona zaidi

WATANZANIA wanahitaji kupata taarifa kamili kuhusu masuala ya corona. Hii ni kwa sababu watu wengi wanapendelea kusikiliza mambo kwa juu juu na kuchukua taarifa ambazo si sahihi badala ya kufuatilia na kuujua ukweli halisi.

Tunasema hivi kwa sababu wapo wanaodhani kuwa corona inawahusu zaidi wazee kwani ndiyo waliofariki huko Italia, China na Hispania kwa mujibu wa madai yao.

Mambo hayaishii hapo, kuna watu wanajidanganya kuwa corona huambukizwa kwa njia ya hewa na wanapoambiwa kuwa inasambaa kupitia kushika majimaji ya mwili wa mgonjwa, kuwa kwenye misongamano, kushikana mikono, kukumbatiana, kushiriki chakula na hata kukaa karibu na walioambukizwa hilo hawalipi umuhimu. Maadamu wamesikia ugonjwa kuambukiza kwa njia ya hewa ndilo wanalolipa kipaumbele.

Hata hivyo, tunasikitika kuwa, Watanzania wengi wameendelea kuamini mambo wanayoyasikia kwenye 'vijiwe vya wazururaji' na ni wachache wanaofuatilia taarifa za ukweli.

Mara nyingi habari za kizushi pengine kutoka kwenye mitandao ndizo zinazosambaa na huenda nusu ya taarifa feki na za uzushi zinazotoka kwenye mitandao na huenezwa kupitia vijiweni.

Tutakumbuka kuwa, mwaka juzi kulikuwa na taarifa za kuzua kuwa kuna nchi inazalisha mchele wa plastiki. Habari hizo zilisambaa duniani kote na karibu Watanzania wote walizisikia na kigezo kimojawapo cha kuutambua mchele wa plastiki kilielezwa kuwa ni kwamba unapoufinyanga kuwa tonge haugandi mkononi.

Watu walikitumia kigezo hicho na kuchunguza vyakula hoteli na wapo baadhi walizua taharuki na kusababisha hofu miongoni mwa wateja na sintofahmu kwa wauza vyakula hivyo.

Taarifa kama hizo zinachukuliwa na kufikishwa vijiweni na kuwafikia Watanzania karibu wote. Licha ya kwamba serikali imeweka utaratibu wa kutoa taarifa za corona kwa utaratibu maalumu, bado wengi wanahitaji kuelimishwa kupitia majukwaa rahisi ya mawasiliano hasa abiria wakiwa kwenye daladala na kutoa matangazo kwenye vituo vya mabasi ili kuwaelimisha wananchi na kufahamisha namna ya kujidhibiti yenyewe na kukabiliana na ugonjwa.

Ni wakati wa asasi mbalimbali za kiraia kusaidia kufanikisha shughuli hizo na hata serikali pia. Tunaona kuwa baada ya kazi nyingi kusimamishwa kama safari za kwenda mikoani kufanya ukaguzi wa shughuli za uzalishaji kwenye viwanda na kampuni au kazi za kutembelea wananchi vijijini, bajeti hiyo inaweza kutumika kufikishia wananchi ujumbe hasa kwenye sekta ya usafiri.


Ni vyema hata kuandaa taarifa muhimu na kuzionyesha kwenye vituo vya mabasi ambako wananchi wengi hupita na kuziona pamoja na kuzisikia.

Tunaona kuwa tuna uwanja mwingine wa kuwasiliana na umma ni barabarani. Hivyo tunashauri kuwa ni vyema kubandika matangazo kuhusu corona kwenye mabango yaliyo pembeni na katikati ya barabara.

Aidha, wananchi wapewe taarifa muhimu kuhusu maambukizi kwa njia nyingine zinazowazunguka, mfano je, unapotoka kazini au popote nje ya nyumbani na umekutana na watu wengi na huko umetumia usafiri wa umma. Je, unatakiwa kuhifadhi wapi mavazi yako nguo pamoja na viatu? Uingie nayo ndani au uache nje? Uzitunzeje? Vipi kuhusu sehemu sahihi za kununua vitakasa mikono? Hii ni muhimu ili kuondoa bidhaa feki, iliripotiwa kwenye vyombo vya habari kuwa kuna nchi jirani zimekamata bidhaa feki sisi tunafanyaje kudhibiti? Wananchi wanasikia kuwa kuna kampuni za kuzalisha vileo zinatengeneza dawa hizo, je, wanaweza kwenda kujinunulia? Zitawafikiaje hasa wale wa pembezoni?

Pia kuna maelezo kuwa Bohari Kuu ya Dawa inahusika na kufanikisha upatikanaji wa vitakasa mikono uwekwe utaratibu wa kuwafikishia wananchi wa makundi yote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Mgogoro ardhi utakufa kwa ubia mwekezaji, mwananchi

UWEKEZAJI unaozingatia ushirikishwaji wa wananchi katika kuamua matumizi ya ardhi kwenye maeneo yao, ndio unahimizwa na serikali kwa lengo la kuepusha migogoro isiyo ya lazima, kati yao na wawekezaji.

Serikali inahimiza utaratibu huo, kutokana na ukweli kwamba mara kadhaa kumejitokeza migogoro ya ardhi katika maeneo ambayo yana uwekezaji, kwa vile wananchi hawaridhishwi na kinachoendelea.

Haifurahishi kuona wananchi wanaumia, pale wanaposhuhudia uvunaji rasilimali kwenye maeneo yao unaendelea, huku wakiwa na maisha duni.

Hivyo, imani yao ni kwamba hawanufaiki na uwekezaji wenyewe.

Hivyo, serikali inataka kuwapo kibali cha jamii katika uvunaji wa rasilimali na makubaliano ya wananchi wenyewe, ili waone moja kwa moja faida ya ama uchimbaji madini au mafuta, hata kukiwapo mradi wa kiwanda mahali hapo.

Ni utaratibu unaohusu uwekezaji wote, hata kama ni kilimo kunakuwapo mikataba kati ya serikali na wawekezaji, bado ni muhimu wananchi wakashirikishwa kama sehemu ya uwekezaji huo, ili waone faida kwa uwazi zaidi.

Hivi karibuni, suala hilo la uwekezaji, lilijadiliwa pia na wadau wa biashara na haki za binadamu, kutoka mikoa mbalimbali nchini, waliokutana jijini Dar es Salaam nao wakahimiza ushirikishwaji wa wananchi.

Mkutano huo uliandaliwa na Asasi ya Biashara na Haki za Binadamu Tanzania (BRHT), ambapo walisema, uwekezaji mwingine unaweza kusababisha uchafuzi au uharibu wa mazingira, hali ambayo ni ukiukwaji wa haki za binadamu, hivyo ni muhimu tathmini ifanyike kabla ya uwekezaji.

Kufanyika kwa hatua hiyo, kunatokana na ukweli wa kuwapo uhusiano mkubwa kati ya biashara na haki za binadamu, hivyo uwekezaji unaozingatia hilo ni muhimu kwa hasa ushirikishwaji wa wananchi wa maeneo husika.

Hicho ndicho serikali inasisitiza na hata wadau hao wanatamani iwe hivyo, ingawa katika mkutano huo ilidaiwa na baadhi ya wadau kuwa viongozi wa serikali kwenye ngazi za vijijini hawazingatii.

Mbali na hilo, hata wanasiasa nao wanadaiwa kuchangia kuwapo kwa sintofahamu hiyo kwa kuwaagiza viongozi wa vijiji kutoa ardhi kwa wawekezaji bila kufuata utaratibu ikiwamo kushirikisha wananchi.

Kama madai hayo yana ukweli ndani yake, basi ipo haja ya kutafuta mbadala utakaowasaidia viongozi hao kutimiza majukumu yao inavyotakiwa, ili kuepusha migogoro ya ardhi isiyo ya lazima.

Inawezekana wengi hawajui sheria zinazohusu mipaka ya majukumu yao au kile ambacho wanatakiwa kukifanya, hivyo ni vyema wakapewa mafunzo maalum ya kuwawezesha kufanya kazi inavyotakiwa.

Kimsingi, ushiriki wa wananchi katika mchakato wa utwaaji ardhi kwa ajili ya uwekezaji ni muhimu na waelimishwe, ili wawe na uelewa wa kutosha kuhusu haki za ardhi na uwekezaji.

Wananchi ni wadau wakubwa katika mchakato wa utwaaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji, kama wasiposhirikishwa, inaweza kutokea migogoro ya ardhi kati ya wanakijiji na wawekezaji, wakulima na wafugaji.

Biashara inayozingatia haki za binadamu itafanikiwa iwapo kutakuwa na ushirikishwaji, kuanzia kwa mwekezaji, viongozi wa serikali na wananchi, lakini mmojawapo akiwekwa pembeni inakuwa tatizo.

Hivyo kunakuwapo na suala la uwekezaji au jambo lolote linalohusu ushirikishwaji, basi viongozi waitishe mikutano ya vijiji kutokana na kuwaambia wananchi kile kinachoendelea kwenye eneo lao.

Ikumbukwe kuwa, migogoro mingi ya ardhi ipo vijijini na kuna wakati inasababishwa na mwingiliano wa matumizi ya ardhi ya kilimo na matumizi mengine.

Vilevile, kuna umuhimu kutambua idadi ya watu imekuwa ikiongezeka, lakini ardhi haiongezeki. Hivyo jitihada za dhati zinatakiwa kuchukuliwa kulinda na kusimamia ardhi kwa uwekezaji wenye manufaa ya pande zote.

Upande mwingine, wenye mifugo mingi wanapaswa kupunguza idadi ya mifugo kwa ajili ya kuepusha migogoro kati yao na wakulima, sambamba na kulinda mazingira.

Upunguzaji idadi ya mifugo, unaweza pia kuepusha mtindo wa kuhama kila mara ambayo imekuwa ikitokea, hasa wakati wa kiangazi wakihangaika huku na kule kutafuta malisho na maji.

Niseme, mabadiliko ya tabianchi yamekuja na mengi, hivyo ni muhimu kuzingatia matumizi ya ardhi kulingana na yanavyoenda.

## Tanesco yaagiza mimea kupisha njia za umeme

**Na Said Hamdani,** LINDI

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco), limewataka watu wote wenye mimea iliyopo kwenye njia za kusafirisha umeme kuridhia kuiondoa ili kuepusha umeme kukatika mara kwa mara.

Hayo yameelezwa na Meneja wa Shirika hilo Kanda ya Kusini, Felician Makotta, alipokuwa akijibu maswali kutoka kwa waandishi wa habari waliofika ofisini kwake kutaka kujua sababu za kukatika umeme mara kwa mara.

Makotta alisema kukatika kwa umeme hakutokani na hitilafu za mitambo, bali ni matawi ya miti ikiwamo ya mimea, miembe, mikorosho, minazi na michungwna mingineyo hasa kipindi cha mvua.

Amesema kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wenye mazao aina hiyo, ambayo njia za umeme zimepitia kutokuwa tayari kutokubaliana na Shirika kwa ajili ya kuondoa sehemu ya mimea husika.

"Upande wetu Shirika tumekuwa tukiwaomba mara kwa mara wananchi kuondoa mimea iliyopo karibu na njia za umeme bila mafanikio," alisema Makotta.

# CAG anusa ulaji umeme wa REA

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini kusuasua kwa mradi wa usambazaji wa umeme vijijini unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA)..

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19, CAG Charles Kichere, anafafanua kuwa, REA ni chombo kinachojitegemea chini ya Wizara ya Nishati na jukumu lake kuu ni kukuza na kuwezesha upatikanaji huduma bora na za kisasa za nishati katika maeneo ya vijijini kwa Tanzania Bara.

CAG anasema amebaini kasi ndogo ya kuunganisha umeme kwa wateja wa maeneo ya vijijini, akieleza kuwa REA iliingia mkataba na makandarasi mbalimbali wa kusambaza na kuweka nyaya za umeme mdogo na wa kati, kusambaza mitambo ya kupoza na kukuza umeme (transformers) na kuwaunganishia umeme wateja katika maeneo yasiyo na umeme kwa upande wa Tanzania Bara chini ya Awamu ya III na ya I kwa kipindi cha muda wa miezi 24.

Hata hivyo, CAG anasema mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa miradi kwa kipindi cha Januari 2020 pamoja na kutembelea maeneo ya ujenzi katika mikoa 13, yalibaini maendeleo ya utekelezaji wa miundombinu yalikuwa yanaendelea vizuri.

Anasema amebaini kulikuwa na kasi ndogo ya uunganishaji wa umeme, ambapo kati ya makadirio ya wateja 8,462 waliotarajiwa kufungiwa umeme wa 3PH, ni wateja 625(7%) tu ndiyo waliounganishwa.

Pia, kati ya wateja 90,606 waliotarajiwa kuunganishwa na umeme wa IPH, ni wateja 21,820 (24%) ndiyo waliounganishwa, huku muda wa mradi wa Juni 2020 ukiwa umebakia miezi sita kukamilika.

CAG anabainisha kuwa mikoa ya Kilimanjaro na Singida imeachwa nyuma katika utekelezaji wa mradi huo, ikiwa imepata umeme huo kwa asilimia tisa tu.

"Menejimenti ilinitaarifu kwamba, kasi ndogo ya kuwaunganishia umeme wateja ilitokana na mambo kadhaa kama kutopatikana kwa nyaya za ABC (Conductors), wateja kukosa utayari wa kufunga nyaya za umeme ndani ya nyumba zao, pamoja na kulipia gharama ya kuunganishiwa umeme.

"Hata hivyo, ni maoni yangu kwamba ucheleweshaji zaidi utaathiri malengo ya serikali ya kuunganisha vijiji vyote kwa umeme wa bei rahisi. Kwa hivyo, napendekeza REA kuwa na mpango wa uhamasishaji ili kuelimisha jamii ya vijijini umuhimu wa umeme katika kuinua uchumi wao," anashauri.

CAG pia pia anapendekeza REA kuwataka makandarasi wote kuwasilisha ratiba za upokeaji wa vifaa na kuhakikisha kufuatwa kwa masharti ya mkataba yanayohusu uwasilishaji wa vifaa kwa wakati.

Pia anasema amebaini ulipaji wa mishahara kwa wafanyakazi wasio hudumu kwenye wakala Sh. milioni 146.021.

Anasema ukaguzi alioufanya kwenye mfumo wa mshahara wa REA kwa mwaka wa fedha 2018/2019, ulibaini kiasi cha Sh. 146, 021,086.40 kimelipwa kwa wafanyakazi wanne kama mshahara wa mwezi Juni mpaka Oktoba 2019.

"Hata hivyo, wafanyakazi hao waligundulika kuwa wamehamia katika taasisi nyingine za serikali. Pia, nilibaini kuwa Menejimenti ya REA ilichelewesha kuijulisha Ofisi ya Rais - Utumishi kuwaondoa watumishi hao kwenye mfumo wa mshahara wa wakala kama inavyothibitika kwenye barua yenye nambari ya utambulisho: CAB/143/166/01/VOL.II/84 & 96 ya Oktoba 4, 2019 na Novemba 7, 2019.

"Hii imechangia sana kutokea kwa matumizi haya yasiyo ya lazima. Menejimenti iliitarifu ofisi yangu kuwa wakala uliagizwa kuwalipa watumishi hao waliohamishwa sababu mishahara yao ilikuwa kwenye bajeti ya wakala kabla ya uhamisho huo. Pia, mishahara yao ilikuwa mikubwa kuliko ya taasisi walizohamishiwa.

"Hata hivyo, ushahidi wa agizo hilo haukuwasilishwa katika kipindi cha ukaguzi. Hivyo ni maoni yangu kuwa udhaifu huu unaweza kusababisha ulipaji wa mara mbili wa mshahara au kuwapo kwa watumishi hewa kama hatua hazitachukuliwa na udhibiti wa ndani wa wakala," anasema.



Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Isimani, Thom Malenga (kulia), akimkabidhi Mganga Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Dk. Samweli Marwa, msaada wa dawa za binadamu zenye thamani ya Sh. milioni 30, zilizotolewa na mbunge wa jimbo hilo, William Lukuvi, kwa ajili ya zahanati na vituo vyote vya afya jimboni humo, ili wananchi wasinunue dawa kipindi hiki cha hofu ya corona. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Rostam atoa vifaa vya mil. 600/- kujikinga corona

**Na Romana Mallya**

MFANYABIASHARA, Rostam Aziz, ameikabidhi Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, mashine, vitakasa mikono na barakoa vyenye thamani ya Sh. milioni 600 kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Rostam alikabidhi vifaa hivyo kwa Mkuu wa Mkoa huo, Paul Makonda, ikiwa ni katika kuunga mkono juhudi za serikali za kupambana na corona.

Msaada huo aliutoa ukiwa ni sehemu ya ahadi yake aliyoitoa wiki iliyopita kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ya kutoa Sh. bilioni moja kusaidia vifaa hivyo katika daladala za jijini Dar es Salaam na visiwani Zanzibar.

Pia, ameongeza mchango wake kwa hospitali mbalimbali kwa kutoa barakoa 70,000 ili kuwasaidia madaktari na wauguzi kujikinga dhidi ya ugonjwa huo.

Kadhalika alitoa galoni 6,000 za lita tano za vitakasa mikono na mashine maalumu za kupuliza dawa ya kupambana na maambukizi ya virusi hivyo.

"Rais (Rais John Magufuli) Machi 22, katika hotuba yake kwa taifa kuhusu janga hili, akitangaza maradhi ya corona, alitupa tahadhari alituambia kwamba pamoja na kuchapa kazi na kuendelea na shughuli zetu za kila siku za kutafuta riziki lazima tuchukue tahadhari kwa kunawa mikono, kutokusanyika na mengineyo.

Rostam alisema tahadhari hizo ni lazima kuzingatiwa kuliko wiki iliyopita au wiki mbili zilizopita.

"Leo hii kwa mara ya kwanza nimevaa hii kitu inaitwa barakoa na hii nimetengenezewa na mama yangu kwa hiyo huna haja ya kwenda kuinunua dukani unachukua shuka au foronya unaifunga na kamba," alisema.

Alisema barakoa inaweza kumuepusha mtu na maradhi mengi na kushauri watu kuchukua nguo zilizochakaa na kuzitengeneza.

"Nimezungumza na madktari wakaniambia ni vyema kuvaa barakoa wakati ninakwenda kwenye msongamano wa watu na wanaweza kutengeneza wenyewe si lazima kununua madukani," alisema.

Mfanyabiashara huyo alitoa wito kwa wafanyabiashara wengine kuisaidia serikali kutoa msaada wa vifaa vya kupambana na corona.

Alisema wafanyabiashara wa nchi nyingine wamekuwa wakifanya hivyo kwa sababu hilo sio jukumu la serikali pekee.

Hata hivyo, Rostam alisema sio lazima mtu awe mfanyabiashara mkubwa ndio ajitolee, hata wenye duka wanaweza kuweka ndoo ya maji na kitakasa mikono.

Akipokea vifaa hivyo, Makonda alisema: "Tunao wajibu wa kulinda nchi yetu na kujilinda wenyewe, wapo watu wanafikiri corona ni kwa ajili ya serikali, na wengine wanasema sisi mpaka ije huku kwetu, ugonjwa huu ni hatari.

"Wakati mwingine unajiuliza hivi mtu mpaka augue nyumbani kwake ndio ajue huu ugonjwa ni hatari, ukiona mtu kama Rostam ameamua kutoa zaidi ya bilioni moja sio kwa sababu ana fedha nyingi, anatamani asife Mtanzania kwa corona."




Mkazi wa Manispaa ya Iringa, Matatizo Mduba, akichukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona kwa kunawa mikono kabla ya kununua magazeti katika eneo la Posta, jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Maalim Seif apongeza uamuzi wa G20

**Na Mwandishi wetu**

MWENYEKITI wa Taifa, ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema kuwa amepokea kwa furaha uamuzi wa nchi zenye uchumi mkubwa duniani (G20), kusimamisha malipo ya madeni ya nchi zinazoendelea ili ziweze kupambana na janga la corona.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na kiongozi huyo, ilipongeza uamuzi huo kuwa ni wa kihistoria na unaojali maslahi mapana ya dunia. "Itakumbukwa kwamba, nilipohutubia Aprili 2020, niliwaeleza Watanzania kuwa tunafanya juhudi ili mataifa yaliyoendelea yakubali kusimamisha malipo ya madeni kwa mwaka mmoja. Nilieleza kuwa Tanzania inatumia takribani Sh. trilioni 4 kila mwaka kuhudumia deni la nje," alisema.

Maalim Seif alisema mataifa ya G20 yametoa nafuu kuanzia Mei mosi, hadi mwishoni mwa mwaka huu, na kwamba ni jambo la kushukuru sana kwa kuwa itatusaidia kukabiliana na athari za janga hilo.

"Natoa wito sasa kwa Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF) kama waratibu wa nafuu hii ya madeni kuhakikisha kuwa nchi zinakuwa na mpango madhubuti wa kugeuza nafuu hii kuwa fursa ya maendeleo ya watu na sio maendeleo ya vitu," alisisitiza.

Aidha, alisema nchi zitakazofaidika na nafuu hii lazima kwanza kuonyesha mpango unaotekelezeka wa kuimarisha sekta ya afya kwa upana wake ikiwamo majisafi na salama, na pia kuwapo kwa mfumo wa uwajibikaji ili kuzuia matumizi mabaya na ubadhirifu wa fedha hizi. "ACT-Wazalendo kama chama pekee kilichoongoza juhudi za kupata nafuu hii, tutakuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa fedha hizi zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa, na kwamba zitakaguliwa na taasisi huru ili kudhibiti mianya ya matumizi mabaya," alisisitiza.

# Kigogo Takukuru, DPP waendelea kujadiliana

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi inayomkabili Mchunguzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Cosmas Batanyika (44), umedai kuwa bado mazungumzo yanaendelea ya kuhusu kukiri kosa kati ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) na ndugu wa mshtakiwa huyo dhidi ya tuhuma za uhujumu uchumi ikiwamo kushawishi rushwa zaidi ya Sh. milioni 300 na kutakatisha Dola za Marekani 20,000.

Kadhalika upande wa Jamhuri umedai kuwa mazunguzmo hayo yakikamilika wataijulisha mahakama.

Madai hayo yalitolewa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoendesha shughuli zake kupitia Mahakama mtandao, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu, baada ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi Godfrey Isaya kuwa na udhuru.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Simon Wankyo, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kwamba mazungumzo kati ya DPP na ndugu yanaendelea yakikamilika Jamhuri utaijulisha mahakama.

Hakimu Chaungu alisema kesi hiyo itatajwa tena Aprili 30, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika mashtaka ya kwanza inadaiwa Februari 9, 2019 eneo la Upanga, mshtakiwa akiwa mwajiriwa wa Takukuru kama Mchunguzi Mkuu, aliomba rushwa ya Sh. milioni 200 kutoka kwa Hussein Gulamal Hasham kwa lengo la kuharibu ushahidi wa tuhuma za kukwepa kodi zilizokuwa chini ya uchunguzi wa mwajiri wake.

Ilidaiwa kuwa Februari 10, 2019, Viwanja vya Maonyesho ya Biashara, Sabasaba vilivyopo Temeke, jijini Dar es Salaam, alijipatia Dola za Marekani 20,000 kutoka kwa Faizal Hasham, kama kishawishi cha kuharibu ushahidi wa tuhuma za kukwepa kodi dhidi ya Hasham zilizokuwa zinafanyiwa uchunguzi na Takukuru.

Pia, ilidaiwa kuwa Februari 13, 2019 katika ofisi za Makao Makuu ya Takukuru, mshtakiwa akiwa mwajiriwa na Mchunguzi Mkuu wa Takukuru, alishawishi rushwa ya Dola za Marekani 50,000 kutoka kwa Thangavelu Nallavan Vall, kama kishawishi cha kuharibu ushahidi wa tuhuma zilizokuwa zinamkabili za kukwepa kodi.

Katika mashtaka ya nne, ilidaiwa kuwa Februari 14, 2019 mtaa wa Haile Selasie, karibu na Merry Brown, Wilaya ya Kinondoni, alishawishi rushwa ya Dola za Marekani 20,000 kutoka kwa Vall kama kishawishi cha kuharibu ushahidi uliokuwa chini ya uchunguzi wake wa kukwepa kodi.

# TPSF yaridhishwa wakulima wa mboga

**Na Enock Charles**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imepongeza ubunifu na uthubutu wa Chama cha Wakulima wa Mboga na Maua (TAHA) kwa kuingia makubaliano katika kusafirisha moja kwa moja bidhaa zao wakati dunia ikipita katika kipindi kigumu cha ugonjwa wa corona.

Chama hicho kimeingia katika makubaliano na Shirika la Ndege la Ethiopia ya kusafirisha moja kwa moja matunda, mboga na maua.

Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, amepongeza makubaliano hayo na kusema ni mfano wa kuigwa wa ubunifu na uthubutu unaochangia sana kuimarisha uchumi wa Tanzania na wa dunia wakati ulimwengu unapitia katika kipindi kigumu cha kiuchumi na kijamii. "TPSF inawapongeza TAHA kupitia kongani ya kilimo kwa kutafuta njia mbadala ili kuhakikisha inaendelea kuwahudumia wateja wake wa Ulaya na duniani pote. Hatua hii itasaidia kulinda ajira za wafanyakazi wengi wa mashambani, mnyororo mzima wa thamani pamoja na wakulima wakubwa na wadogo wanaotegemea kilimo hiki kuendesha maisha yao," amesema Ngalula.

Ameipongeza serikali kwa kuunga mkono juhudi za wanachama wa TPSF, na kuziomba taasisi katika sekta ya usafirishaji kutoa huduma kwa ufanisi ili kupunguza gharama kusudi Tanzania inufaike na mkataba ambao umefikiwa. Aidha ameziomba kongani nyingine za TPSF kubuni mikakati ya kuwasaidia wafanyabiashara kuendelea kuwa na kipato.

Alitaja majukumu matatu ya wanachama wa TPSF wakati huu ni kutoa elimu ya kuzuia maambukizi, kulinda ajira na kuhakikisha huduma muhimu kama upatikanaji wa vyakula na zingine zinaendelea.

Aliwasihi Watanzania kujikita katika kilimo kwani matunda na mboga vinahitajika kwa wingi ndani na nje ya nchi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TAHA, Dk. Jacqueline Mkindi, alisema kupatikana kwa ndege ya kusafirisha mazao katika kipindi hiki ni fursa kubwa kwa wazalishaji wa bidhaa za mboga na matunda wa Tanzania na kuwaomba wazalishe bidhaa kwa wingi kwa kuwa kuna uhakika wa usafirishaji bidhaa hizo nje.

# Mwandishi wa DW asimulia alivyopata corona

Na Romana Mallya

MWANDISHI wa habari wa Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Ujerumani (DW), visiwani Zanzibar, Salma Said, amethibitisha kukutwa na virusi vya corona baada ya awali kupata dalili za ugonjwa huo.

Akizungumza na chombo kimoja cha habari, Salma alisema alianza kujisikia uchovu na koo kuwasha.

"Mbavu zilikuwa zinanibana, nilikuwa siwezi kupumua vizuri, kwa siku mbili nilikuwa na homa mfululizo na kichwa kilikuwa kinaniuma.

"Viungo navyo vilikuwa vinaniuma kama vile mtu mwenye malaria au homa kali ya mapafu, niliwasiliana na daktari akaniambia kama nina dalili hizo ni za corona, ndipo akawaambia madaktari wakaja wakachukua vipimo na majibu yameonyesha nina corona."

Salma alisema kwa muda wa siku 12 hakutoka ndani aliamua kupumzika nyumbani akiendelea kufanya kazi.

"Utaratibu wa Deutsche Welle (DW), tuliamua watu wafanye kazi wakiwa nyumbani ili wajilinde zaidi, nilikuwa Dar es Salaam kwa hizo siku 12, nilitoka siku moja tu kwenda Kariakoo na nilivyorudi Aprili 7, nilifikia nyumbani sikutoka.

"Siku ya pili (Aprili 8), nilikwenda ofisini kwangu nikawa na wenzangu pale, jioni nikaanza kusikia maumivu ya viungo, homa kali na kichwa kuuma kwa muda wa siku mbili.

"Nilikuwa nakohoa kidogo ila kooni nilihisi kunawasha na kuwa na kifua kikavu, hii ndiyo iliyonitia wasiwasi, lakini ile homa na kupumua niliona ni kawaida kwa sababu nina tatizo la pumzi, nina tatizo la moyo."

Salma alitoa simulizi hiyo kabla ya kuchukuliwa kupelekwa kwenye kituo maalum cha wagonjwa wa corona.

"Tangu nimerudi kutoka Dar es Salaam, nilikuwa nipo nyumbani peke yangu, watu ambao nilichangamana nao ni wale wale wa ofisini nimeshatoa taarifa zao kwa maofisa wa afya," alisema.



Mbeba mizigo katika soko la Mabibo maarufu kama Mahakama ya Ndizi, jijini Dar es Salaam, akiwa miguu mitupu huku akipita kwenye matope yaliyolizingira soko hilo, jana, kutokana na mvua inayoendelea kunyesha. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TIC: Wavamizi maeneo ya uwekezaji waondoke

Na Mwandishi Wetu

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Geoffrey Mwambe, amewataka watu waliovamia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji na ambayo yapo chini ya kituo hicho kuondoka bila shuruti ili kutoa nafasi kwa shughuli zilizokusudiwa. Akizungumza mara baada ya kutembelea mashamba yenye ukubwa hekta zaidi ya 13.5 yaliyotengwa na serikali kwa ajili ya kilimo cha michikichi wilayani Uvinza ambapo maeneo hayo yamevamiwa, Mwambe aliwataka wavamizi kuondoka mara moja kwenye mashamba hayo na kupisha kuendelea kwa shughuli iliyokusudiwa. "Mashamba haya mawili yana hekta 3,249.76 na 10,529.86 yametengwa na serikali kwaajili ya uwekezaji wa kilimo cha zao la michikichi ili kuzalisha mafuta ya kula ya mawese na kuondokana na changamoto ya kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi," alisema.

Kwa mujibu wa Mwambe, takwimu za Wizara ya Kilimo, Tanzania inaagiza tani 400,000) za mafuta ya mawese, huku ikitumia zaidi ya Sh. bilioni 600 kila mwaka kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi ili kufidia pengo la uhaba wa bidhaa hiyo nchini.

Mwambe alisema serikali kwa kuliona hilo, iliamua kuliongeza zao la michikichi kuwa ni miongoni mwa mazao saba ya kimkakati ikiwamo pamba, chai, kahawa, korosho, katani na tumbaku. "Mpango wa nchi kwa sasa ni kuepuka kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi pamoja na kupunguza gharama kubwa ya kuagiza bidhaa hiyo, bado usalama wake unatiliwa shaka na pia hutumia fedha nyingi za kigeni badala ya kuzielekeza katika matumizi mengine ya msingi.Katika ziara hiyo, Mwambe alikutana Mkuu wa Mkoa huo, Brigedia Jenerali mstaafu, Emmanuel Maganga na Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Mwanamvua Mrindoko, ambapo walizungumza na kupanga mikakati ya kuwaondoa wavamizi wote na kuyalinda maeneo hayo.

"Nimekuja kwa ajili ya kuangalia na kufanya majadiliano na uongozi wa mkoa na wilaya kuhusu namna bora ya kuyalinda mashamba yaliyotengwa na serikali kwa ajili ya uwekezaji," alisema.

Brigedia Jenerali Maganga alisema kazi iliyopo mbele yake ni kuhakikisha ulinzi unaongezwa kwenye maeneo hayo ili yasivamiwe zaidi kwani sula la uvamizi linaathiri shughuli nyingi za uwekezaji katika mkoa wake.

Aliagiza wote waliovamia maeneo ya uwekezaji mkoani humo kuondoka mara moja, vinginevyo watapoteza mali zao na kutoa wito kwa wananchi kutoingia kwenye eneo au pori wanaloliona bila kufuata

## Udongo wa kujikinga na magonjwa wagunduliwa

Na Mwandishi Wetu

TAASISI inayojihusisha na afya ya jamii ya Afrika Mashariki, Tarkeu Wema Association, imetambulisha udongo wenye maajabu (amazing green soil) uliothibitishwa kuwa na uwezo wa kumkinga mwanadamu dhidi ya maradhi mbalimbali ukiwamo ugonjwa wa Covid-19.

Taasisi hiyo ni umoja wa wahadhiri na wanafunzi kutoka vyuo vikuu Afrika Mashariki, kikiwamo Chuo Kikuu Dar es Salaam, St. Augustine, Mzumbe na Tumaini, kutoka Tanzania na Chuo Kikuu Nairobi na Kenyatta nchini Kenya, Chuo Kikuu Butare na Kigali nchini Rwanda na Chuo Kikuu Makerere nchini Uganda.

Taarifa iliyotolewa na Taasisi hiyo imesema mtaalamu na mtafiti wa viumbe na ardhi, Dk. Riser Nitsch, toka Chuo Kikuu cha Muenster nchini Ujerumani, utafiti wake umegundua aina saba tofauti za udongo na kati ya hizo sita za kawaida, ukiwamo unaoliwa na kinamama wajawazito na wanyama wa porini wakitafuta madini yaliyomo.

Ilisema aina saba ni udongo wa ajabu unaopatikana katikati ya nchi ya Israel na Lebanon na kuthibitika kuwa una madini mbalimbali ya asili yanayoweza kusaidia kuimarisha afya ya mwanadamu.

Taarifa hiyo ilisema faida za udongo huo ni nyingi, lakini baadhi ni kiosha asilia kutoa kemikali /sumu ndani ya mwili, hudhibiti vyanzo vyote vya kansa, huzuia kusambaa kwa kansa na magonjwa mengine mwilini na huzibua mirija na kurekebisha mfumo wa uzazi na kuwa msaada kwa wanawake wanaoshindwa kushika ujauzito.

Faida nyingine ni kuondoa aina tofauti za uvimbe mwilini na kudhibiti utokeaji wa viumbe nyingine, kuimarisha neva za mwili, hivyo kusaidia watu wazima na wazee kujimudu wanapohisi haja ndogo.

Vile vile udongo huo wa maajabu una madini ya calcium, zinc na madini ya chuma asilia ambayo huimarisha mifupa na meno.

Taarifa hiyo ilisema kulingana na ushauri wa mtaalamu huyo, teknolojia huja kwa haraka na haizuiliki kulingana na faida zake na kwamba technolojia hiyo hiyo watu wasipokuwa makini, husababisha madhara ya kiafya kupitia mionzi, vyakula na vinywaji vya kisasa vyenye kemikali.

"Ushauri wa kiafya, kama tunavyosafirisha miili yetu kwa nje, pia yatupasa kujisafisha kwa ndani kuondoa kemikali hizo. Kwa sababu huzalisha maaskari wanaoimarisha kinga za mwili kwa wingi," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa, Dk. Riser anashauri ni vyema kutumia `Amazing soil' hususani kwa kipindi hiki cha janga la Covid-19.

Pia, taarifa inasema Dk. Riser, alipoulizwa kwa nini udongo huo haupatikani sehemu zingine, alijibu kuwa hupatikana Shetula pekee ambako ni katikati ya Israel na Lebanon, kwa sababu ndiko penye madini ya aina yake na bora kwa afya ya binadamu.

Taarifa inasema udongo huo hauna madhara kwa binadamu kwa sababu ni halisi na ulifanyiwa utafiti na wataalamu wabobezi.

Ilisema mtu anaweza kuwasiliana na Tarkeu Wema Association East Afrika, kwa kupatiwa huduma na sio biashara kupitia anuani;

Pioneer House Kenyetta Avenue 3rd Flr, Rm 317 Anuani: SLP 24146. 00100, Nairobi, kwa namba ya simu Kenya +254 735220133, au mwakilishi wa Tanzania

Dk. Annely Godable kwa namba 0787 541 703, 0742365818.

# Tamisemi yafafanua mpaka Manispaa Moro, Mvomero

MBUNGE wa Morogoro Mjini (CCM), Abdulaziz Abood (pichani) amehoji serikali itamaliza lini mgogoro kati ya Manispaa ya Morogoro na Halmashauri ya Mvomero juu ya Mtaa wa Maili Kumi na Nane ambao uko mjini.

Akiuliza swali bungeni jana kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Abood alihoji: "Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro huu ambao kimsingi mtaa huu upo mjini?"

Katika majibu yaliyotolewa na Ofisi hiyo, ilisema utatuzi wa mgogoro huo ulifanyika, ambapo uongozi wa Mkoa wa Morogoro ulifanya kikao cha pamoja Oktoba 2, mwaka 2018 kilichohusisha Halmashauri zote mbili.

Ilisema katika kikao hicho walikubaliana kufuta Mtaa wa Kumi na Nane ili eneo hilo liunganishwe katika kijiji cha Wami Sokoine kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero.

"Marekebisho haya yameshafanyika kupitia Tangazo la Serikali Na. 536 la tarehe 19/07/2019 la Mamlaka za Miji na Tangazo la Serikali Na. 537 la tarehe 19/07/2019 la Mamlaka za Wilaya kwa kuufuta Mtaa wa Maili Kumi na Nane uliokuwa katika kata ya Mkundi iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ili kuwa sehemu ya eneo la Kijiji cha Wami Sokoine," ilisema.



# Ujenzi wa nyumba 450 kukabili kero za askari Polisi



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imesema Serikali inatambua uhaba wa makazi kwa askari wa Jeshi la Polisi nchini ambapo kwa sasa ipo kwenye ujenzi wa nyumba 450 mikoani.

Hayo yalibainishwa jana bungeni katika majibu yaliyotolewa na Wizara hiyo kwenye swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Anna Gidalya.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema jeshi hilo ni mhimili unaolinda amani pamoja na usalama wa raia na mali zao.

"Kwa kuwa Serikali imeanzisha vituo vya Polisi katika tarafa na kata mbalimbali bila kuwa na nyumba za kuishi je, serikali ina mkakati gani wa kuwajengea nyumba za kuishi na vituo ili waondokane na kero na hofu kulingana na uhalisia wa mazingira yao ya kazi?," alihoji.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema zipo juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na serikali katika kukabiliana na tatizo la makazi ya askari kwa nchi nzima.

"Mathalani, ujenzi wa jumla ya nyumba 450 katika mikoa Tanzania Bara na Zanzibar ambapo baadae nyumba zitajengwa katika wilaya na hatimaye kwenye Tarafa na Kata," ilisema.

Aidha, ilisema Jeshi hilo linao utaratibu wa kulipa fedha za makazi kwa askari ambaye atakuwa anaishi nje ya kambi ya Jeshi la Polisi, hivyo kumuwezesha kumudu gharama za pango.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

## Mradi kuboresha makazi duni mbioni kukamilika

BUNGE limeelezwa kuwa, kwa sasa Serikali inakamilisha mradi mkubwa wa kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini kama sehemu ya mkakati wa kuboresha makazi duni mijini na vijijini.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ilibainisha hayo bungeni jana kwenye swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Martha Umbula (pichani chini).

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema moja ya vigezo vya kupima umaskini wa wananchi ni pamoja na hali duni ya makazi na maskani ya watu wake. "Katika Mkoa wa Manyara bado wapo wananchi wenye makazi duni ya udongo na nyasi pamoja na vibanda vya kuishi visivyokidhi haja," alisema.

Alihoji serikali imeweka mikakati gani ya kuboresha makazi duni ya wananchi ikiwemo Mkoa wa Manyara?

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilielezwa katika kutekeleza mikakati ya kuboresha makazi duni nchini, Serikali ilianzisha Wakala wa Utafiti wa Vifaa vya Ujenzi na Nyumba Bora (NHBRA).

"Lengo ni kufanya utafiti wa vifaa vya ujenzi vinavyopatikana hapa nchini na kuviboresha ili viweze kutumika kujenga nyumba imara na bora," ilisema.

Ilitoa mfano matumizi ya tofali za udongo kwa kutumia saruji kidogo (Soil stabilized bricks), ujenzi kwa kufungamanisha tofali (Interlocking Bricks) bila saruji, vigae vinavyotengenezwa kwa mchanganyiko wa mchanga, saruji na nyuzi za katani na mashine za kuzalisha vifaa hivyo.

Aidha, ilisema elimu ya matumizi ya teknolojia hiyo imetolewa kwa Halmashauri nchini.

Pia, ilisema Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) limekuwa likitoa ushauri na mafunzo kwa vikundi vya ushirika wa nyumba juu ya namna ya kujenga nyumba za gharama nafuu.

"Hivyo, Serikali inashauri wananchi kujiunga na kuanzisha vikundi vya ushirika wa nyumba ili kupatiwa elimu ya matumizi ya vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu vilivyofanyiwa utafiti na wakala," ilisema.

Kadhalika, ilisema katika mwaka wa fedha 2018/19, Serikali kupitia Wizara hiyo ilizikopesha Halmashauri 24 jumla ya Sh. bilioni 6.28 kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi ambapo jumla ya viwanja 40,651 vimepimwa na umilikishaji unaendelea.



BUFE
Ijumaa Aprili 17, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

Ujue umoja wa walemavu wenye mashine ya kusaga, shida palepale

BIASHARA

# Maswali mazito Ushetu, ukoje utata Rea kuwaweka kando umeme wao?

## WAZIRI, RAS, DIWANI WAJIBU....

**Na Neema Sawaka**

WAFANYABIASHARA na wenye viwanda vidogo katika Kata ya Ulowa ndani ya Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, wanalalamika kukosa nishati umeme, hali inayowahamishia katika matumizi ya jenereta zenye gharama kubwa na tija ndogo.

Katika hesabu zao wanadai, chanzo cha jenereta inawagharimu fedha Sh. 500 kwa kuhudimia balbu moja na anayetumia pamoja na friji au mfanyabiashara, anaingia bajeti ya Sh. 6000 kwa siku .

Julius Masanja na Baraka Jeremiah, ni wamiliki wa viwanda vidogo vya kutengeneza mashine za kukoboa mahindi, karanga, pia kutengeneza vitanda vya chuma, analalamika inamwia ngumu kikazi anapokosa umeme.

Masanja anasema kutumia mashine za ukoboaji, zinamfanya atumie nguvu kuhuzidumia, jambo linaowaweka pagumu hata wanashindwa kuwaachia wake zao nyenzo hizo za uzalishaji mali.

"Ungekuwepo umeme, ufanyaji kazi wa mashine za kukoboa ungekuwa rahisi. Tunaiomba serikali kututatulia changamoto hii, kwani tunaonekana kuteseka wakati tunatekeleza sera ya Uchumi wa Viwanda, ambayo ndio tumeanzisha lakini huduma muhimu hakuna," analalamika Masanja.

Jeremiah analalamika, matumizi ya jenereta yamefanya kuongezeka bei ya bidhaa zao, kwani gharama za kuendesha ziko juu sana, mziiz mkuu ni kwenye pesa inayotumika kwenye mafuta.

"Wateja wamekuwa wakitukimbia kwa madai vitu vyetu tunauza kwa bei kubwa, tofauti na maeneo yenye nishati ya umeme utakuta kitu cha laki sita tunakiuza laki tisa, wateja wanakataa tunashinda na vitu vyetu kwa kukosa wateja sababu ya bei kubwa, " anasema Jeremiah.

Kulwa Shija, mmiliki wa mashine ya kupukuchua mahindi, anasema wanatumia gharama ya Sh. 2000 kwa gunia moja, huku mmiliki wa kituo cha mafuta katika kijiji Namba Nne, Safari Manjala anasema changamoto anayoipata ni gharama kubwa za kuendesha biashara.

Anasema, atumia Sh. 790,000 kwa ajili ya mafuta ya kuendeshea jenereta kila mwezi na anafafanua kama ungekuwepo umeme wa kawaida, gharama ingeshuka hadi Sh. 90,000 kwa mwezi, hivyo anaomba serikali kuharakisha uwepo wa umeme wa Rea haraka.

Mwenyekiti wa kijiji cha Namba Nne Paul Shinji anasema wana mahitaji mengi ya shughuli zinazohitaji umeme na anaiomba serikali kuwakumbuka hataka katika eneo hilo, waondokane na adha ya jenereta iliyopo sasa.



Mmiliki wa mashine ya kumenya karanga katika kata ya Ulowa, Julius Masanja, na mteja wake aliyeinama, James Masola, wakiwa katika mashine inatyotumia mafuta, wakiendelea na kazi. **PICHA: NEEMA SAWAKA.**

**DIWANI WA ULOWA**

Diwani wa Kata ya Ulowa, Paschal Mayenga, anakiri changamoto ya nishati ya umeme ilikwishawasilishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani na majibu yalitoka 'mpaka awamu nyingine.'

Mayenga anasema kuwa katika kata hiyo ni kijiji kimoja cha Bugera ndicho kimepatiwa na umeme wa Rea na kiko umbali wa kilomita kumi kutoka Ulowa Namba Nne, ambayo anadai inaongoza kwa kuchangia mapato kwenye halmashauri.

"Tumekuwa tukitumia umeme wa jenereta ambao unatumika kwa kwa kufanya zamu, ikiwa unawashwa saa tatu mpaka saa saba mchana unazimwa na baadaye unawashwa saa saba hadi saa tisa jioni, hali hiyo inawafanya wafanyabiashara na viwanda vidogo kutumia gharama kubwa," anasema.

Mayenga anasema yaliyofanywa na Wizara ya Nishati walipohudhuria kikao cha Baraza la Madiwani, walieleza kijiji Namba Nne Ulowa kina wateja 750 na kijiji cha Bugera kilichopitiwa na umeme awamu ni makadirio ya wateja 16 pekee.

**VIONGOZI WA SHINYANGA**

Katibu Tawala wa Mkoa Shinyanga, Albert Msovela, anasema wanapata nishati umeme kutoka katika mkongo wa Taifa wenye kilovoti 220 ila umeshindwa kufikia maeneo yote, klwa jumla kukiwapo viwanda 727, katika mgawanyo; vikubwa 13, vya kati 10 na vidogo 704 , vyote vinahitaji nishati hiyo.

"Mkoa huu una wilaya tatu. Wilaya ya Kahama katika maeneo 21 bado hayajapata nishati ya umeme, ambayo wawekezaji wanategemea umeme wa uhakika, Ukikatika mara kwa mara unaweza kuleta shida katika uwekezaji wao," anasema Msovela.

Mbunge wa Ushetu, Elias Kwandikwa, anasema umeme wa Rea umeanza kuwaka katika baadhi ya maeneo na vijiji vya Kata ya Ulowa vitafikiwa awamu nyingine, mpango wa uliolenga kuvifikia vijiji 54.

**WAZIRI KALEMANI**

Waziri wa Nishati Dk.Medard Kalemani, anasema mkoa wa Shinyanga kupitia Mkongo wa Taifa katika kituo cha Ibadakuli chenye megawati 90 na hadi sasa mkoa unatumia megawati 60 na matarajio ya wizara, ni kusambazia vijiji vyote nishati ya umeme.

Dk. Kalemani anasema katika awamu ya tatu ya utekelezaji wa Rea, mkoa wa Shinyangayrtafikiwa na huduma za umeme wa Rea katika jumla ya vijiji 140 na Halmashauri ya Ushetu imepewa kipaumbele zaidi ya kupitiwa na vijiji 54 sawa na asilimia 38.57 ay wastani wa theluthi moja.

# Ujue umoja wa walemavu wenye mashine ya kusaga, shida palepale

## ■ Malighafi mtihani, mkopo nao historia

**Na Beatrice Philemon**

HAWA ni wajasiriamali walemavu wenye kikundi kinachojulikana kama 'Umoja wa Kusaidiana Walemavu.' Jumla yao wapo 35 na wanapatikana katika mtaa wa Lukooni, Chanika, nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Vita na kilio chao cha kupata mtaji wa kuwakwamua kiuchumi kwa namna fulani imefanikiwa, kwa maana ya kufadhiliwa mashine ya kusaga nafaka.Waswahili wana usemi 'mwanzo mzuri.' Lakini bado wamekwama, mtihani wa sasa ni mtaji wa kuendesha biashara hiyo.

Mashine hiyo ni msaada kutoka kwa aliyekuwa Meya wa Wilaya ya Ilala, Jerry Slaa, lakini bado wanashindwa kuiendeleza mradi kwa sababu ya mtaji 'umepelea.'

Kipi tena? Mwanachama Saidi Kwaro, ambaye wenzake wamemkasimu kuendesha mashine hiyo, anayesaidiana na Mwenyekiti, pia Mwanzilishi wa chama, Salma Ramadhani.

Hoja ni kwamba, kwa sasa kwamba wateja wao ni wasagaji wadogo wa vyakula vya nafaka za watoto, ambazo hazina tija kwa mapato ya kutosha.

Saidi anasema kinachowakwamisha ni kukosekana mtaji wa kununua malighafi, ambayo ungewasaidia kuuza bidhaa za nafaka sokoni, hata wakafaidika kimapato na kuwaletea mabadiliko ya maisha.

"Tunaomba mtu anayeweza kutupatia au kutukopesha mahindi, hata kwa mkataba ili tuweze kusaga unga na kuuza kwa ajili ya kujiongezea kipato, kusaidia watoto wetu kupata elimu nzuri na huduma nyingine za kijami," anasema.

Hata hivyo anakiri, mradi umewasaidia kiasi wanapoumwa au mikasa ya vifo, ndiyo fedha zinatoka kwenye akiba ya mradi.

Saidi anatoa ombi la chama ni kumpata mdau wa kujitokeza kuwasaidia kuwanunulia pikipiki aina ya Bajaji au Toyo, ibebe mali zao na kuzisambaza bidhaa kwenda katika masoko na Mwenyekiti Salma anaendeleza, akitamka:

" Tulianzisha chama mwaka 2004 kwa ajili ya kusaidiana, kutambuana na kupeana changamoto mbalimbali kulingana na hali zetu."

Anafafanua ombi lao ni mradi kusaidiwa malighafi ya mahindi au mbadala wa pesa za kununua, ili kuwezesha mradi ukue.

### WANAPOKWAMA

Saidi anasema mwaka jana, chama kiliomba mkopo wenye thamani ya Sh. milioni nane kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Ilala na walifanikiwa kupata Sh. milioni tatu, walizotumia katika mgawo; Sh. 500,000 za kununua vifaa vya matengenezo ya mashine ya kusaga, umeme na fedha zilizobaki walinunua mahindi.

"Tulipokwenda sokoni tulichagua mahindi mazuri, baadae tuliamua kurudi nyumbani," anaanzisha simulizi za kusikitisha na anaendeleza:

"Wafanyabiashara walipoleta mahindi katika eneo letu la kusaga nafaka tulipofungua magunia, mahindi mengi yalikuwa mabovu sana, hayajakauka vizuri na tulishindwa kuyarudisha kwa sababu tulikuwa tumeishayafungua."

Anasema baadaye waliamua kuchagua mahindi mazuri, ila walipata hasara kubwa wakati wa kusaga gunia moja lililotoa kilo 45 na kilo 10 ya unga walikuwa wanauza kwa bei ya Sh. 7500, kilo tano Sh. 5000 na kilo 25 waliuza Sh.15,000.

Saidi anasema fedha walizopata walitumia kununua vifaa vya mashine za kusaga na waliwalipa mafundi watatu, pia kuhudumia miundombinu ya umeme iliyokuwa inasumbua, hata kukwaza mashine za kufanya kazi.

"Mpaka sasa 'stata' tumetengeneza moja na nyingine bado, fundi anasema atuunganishie waya, halafu tukipata hela atakuja kufunga tena stata," anaeleza.



Mwenyekiti wa Umoja wa Kusaidiana Walemavu Chanika, Salma Ramadhan, akimimina mahindi, kusaga unga wa watoto. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON.**

> **"Wafanyabiashara walipoleta mahindi katika eneo letu la kusaga nafaka tulipofungua magunia, mahindi mengi yalikuwa mabovu sana, hayajakauka vizuri na tulishindwa kuyarudisha kwa sababu tulikuwa tumeishayafungua**

### OMBI MKOPO

Saidi anasema ombi lao ni ufadhili wa kununuliwa mahindi, wao watasaga unga na kupaki vizuri kwenye mifuko yenye ubora na kisha wanasambaza kwa wananchi.

Mwanachama Mwita Marwa, anasema baada ya kuona maisha magumu, walibuni mbinu ya kuunda kikundi kidogo cha watu watano wanachokiita Tujitegemee Group, ili waweze kupata mkopo wa Bajaji.

Anasema, wameshasajili chama chao, lakini tangu mwaka jana walipeleka katiba yao katika uongozi wa Manispaa ya Ilala na waliomba mkopo wa Bajaji mpaka sasa hivi hawajapata.

"Tukifika Manispaa ya Ilala tunaambiwa nendeni mkae kwanza tutawapigia simu na mimi kila mwezi lazima niende manispaa kuangalia tumefikia hatua ipi ya kupatiwa mkopo," anaeleza.

Analalamika kwamba, katika ufuatiliaji huo wanakutana na majibu ya ukali kutoka kwa ofisa mmoja mwenye dhamana (amemtaja), akidai anawakatalia pindi wanapoomba kuonana na viongozi wanaohusika na masuala ya mikopo kwa madai "wanaomba hela nyingi."

Mwita anafafanua waliwasilisha ombi la mkopo tarehe 19 Septemba, mwaka jana, na wakatakiwa kufungua akaunti, jambo walilotekeleza tangu Oktoba 17, mwaka jana na baada ya hapo, anadai ndio kimya cha majibu kimetawala.

### SHIDA BINAFSI

Katika kauli ya masikitiko, Saidi anasema ukosefu wa malighafi kuendeleza mradi unaangukia hata katika maisha binafsi wanapata dhiki ya mlo mmoja kwa siku.

Pia, analalamika wanachama wanapata shida ya kupata huduma za afya, hata kupeleka watoto shule, kwa sababu kipato kimekwama.

Anasema, walijaribu kwenda kwa Mkuu wa Wilaya ya Ilala zaidi ya mara tatu, kufauta msaada wa Bima ya Afya, lakini hawakufanikiwa.

"Hivi sasa unaweza kuumwa au mtoto akaumwa lakini kwa kuwa hakuna fedha, basi mtoto au wewe mwenyewe utaendelea kukaa nyumbani na ugonjwa wako," anasema.

Pia, Saidi analalamika kwa sasa kodi za nyumba za kupanga zipo juu sana, akifafanua:"Kutokana na tatizo hilo, hivi sasa tunaishi vibaya sana hata kula kwenyewe ni shida."

### MWEKA HAZINA

Mweka Hazina wa Umoja wa Kusaidiana Walemavu Fidelis Mabeche, anasema hali yao wanachama wote kwa jumla wana changamoto nyingi sana,ilhali wengi wana hitilafu za viungo na kiuchumi hawapo vizuri, wanashindwa kukimbizana na soko.

Anataja eneo lingine la matatizo kwao ni kuwa, baadhi wana watoto wenye ulemavu huku hawapati fursa za kielimu kwa usahihi ua kukosa kabisa, kama ilivyo kwa watoto wasi na matatizo hayo.

"Mlemavu anaweza kuugua akashindwa kwenda hospitali, kwa sababu akienda hospitali hana hela na hakuna atakayemuangalia, ingawa serikali ina sera ya kusaidia walemavu, lakini hatupati," analalamika.

Mabeche anasema, mpaka sasa umoja wao una watoto watatu wasiopata fursa za elimu na huduma nyinginezo.



Hamis Dilongore, akisaga unga wa lishe kwa ajili ya chakula cha watoto katika mashine yao.

## DK. SOPHIA KASHENGE

# Bosi Wakala wa Mbegu anayeeleza namna alizeti itamaliza shida mafuta

- Vinara kimataifa, kujitosheleza 40% tu
- Naibu Waziri aja na 'tunaondoka vipi'

**Na Christina Haule, Morogoro**

KATIKA kutimiza ahadi ya Serikali ya kuingiza zao la alizeti kwenye mazao ya kimkakati nchini, jumla ya tani 5000 zinahitajika kwa mwaka kukidhi mahitaji. Ili kufikia azma hiyo, iko wazi kunahitajika upanuzi wa mashamba kuboresha maeneo yaliyopo.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mbegu nchini (ASA), Dk. Sophia Kashenge, anawashauri walimaji waboreshe maeneo yao na alishaongea na wakuu wa wilaya yalipo mashamba tisa ya wakala wake, kuboresha ulinzi wake, kukabiliana na wavamizi wa maeneo.

Dk. Kashenge anasema, licha ya kuanza uzalishaji wa zao hilo wakiwa na jumla ya tani 74 katika mwaka 2017/18, mpaka sasa wana tani 243, baada ya zao hilo kupewa kipaumbele cha kuingizwa kwenye mazao ya kimkakati.

Anasema ongezeko la uzalishaji linafanya uingizaji wa mafuta ya kula yatokanayo na alizeti kutoka nje ya nchi inaumia na wanategemea kuongeza uzalishaji zaidi, kutokana na hamasa iliyopo kukuza kilimo tajwa.

Mtendaji huyo anasema, kuna jumla ya hekta 7,600 zinazotumika kupandwa alizeti nchi nzima na upatikanaji wa teknolojia za uzalishaji uko kwa kiwango cha asilimia 43 hivi sasa.

Dk. Kashenge anasema tani 2,875 ndizo zinahitajika nchini mwaka huu, na iwapo watazalisha tani 243 na kuingiza tani 10, bado hawafikii hata asilimia 10 ya lengo la mahitaji yaliyopo katika kuzalisha mafuta.

Dk. Kashenge anasema takwimu za Beniki Kuu ya Tanzania (BoT), zinaonyesha upatikanaji mafuta ya kula nchini ni asilimia 40 na asilimia 60 ni mafuta kutoka nje ya nchi.

Anasema, asilimia 30 ya uzalishaji mafuta nchini, chanzo chake ni alizeti na Tanzania inashika nafasi ya 11 duniani na barani Afrika ni ya pili. Ukraine ndio inayoongoza kote.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mbegu, anasema mkakati ulioko sasa ni kuelekea kupunguza uingizaji mafuta ya nje ya nchi na kuwekeza katika kilimo cha alizeti, ili kurudisha pesa nchini na kukuza uchumi wa nchi.

Dk. Kashenge anasema changamoto iliyopo sasa kwa wakulima ni kulima eneo kubwa na kupata mazao kidogo.

Anasema, kuvuna kiasi kidogo kunatokana na sababu mbalimbali ikiwamo matumizi ya mbegu za kienyeji, ukame, ndege wavamizi na hali hiyo huyakumba mazao yaliyo mengi.

Pia, anazungumzia uzalishaji katika viwanda vya ndani vya mafuta unakuwa mdogo kwa sababu ya uhaba wa mbegu kitaifa, huku ukanda wa kati kwa mikoa ya Dodoma na Singida ambako ndiko kwenye ardhi bora , bado kunasuasua.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akikagua ghala la kuhifadhia mbegu la Wakala wa Mbegu Tanzania, katika ziara yake mkoani humo. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE**.

Hivyo anasema, changamoto hizo zinajitokeza kutokana na ukosefu wa usimamizi wa kutosha na kwamba wakulima wanaendesha kilimo, bila ya kufuata taratibu bora za uzalishaji mazao, huku kuwepo maofisa ugani katika kila wilaya na kijiji, kunasaidia kumfanya mkulima aweze kutambua mbegu bora zinazomuongezea uzalishaji.

Anawashauri wakulima wa Dodoma na Singida, watumie mbegu bora za alizeti zilizothibitishwa kitafiti kuwa na uwezo wa kuzalishaji kiwango kikubwa cha mafuta na mashudu yake yana vitamini na mbegu zake ni nzito.

Kwa mujibu wa Dk. Kashenge, kupitia utafiti wa mwaka 2017/18 wameanza kupata mbegu bora iliyopandisha kiwango cha mafuta nchini kutoka asilimia 18 hadi 23 za awali zinazopita asilimia 32 hadi 40.

Anasema mbegu za mwanzoni zilizalisha kwa ubora, licha ya kupingwa na sasa kuna mtazamo wa kutumika kutokana uhalisia wa ubora wake.

Dk. Kashenge anaendelea kuwa, takwimu za kiutafiti kwa hekta ambayo ni sawa na ekari 2.5 hata mkulima asipotumia mbolea, bado kuna uwezo wa kuzalisha tani 1.5, kwa kutumia mbegu za uzito wa gramu 6.8.

**SHAMBA DARASA**

Dk. Kashenge anasema ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji inaikwaza michakato ya tija ya wakala wa mbegu na wako katika mtazamo wakipata nguvu kuingia katika kilimo cha umwagiliaji na wakiwa na matrekta ya kutosha, wana uwezo wa kuzalisha na kufikia tani 900, hali inayokuza upatikanaji wa mafuta nchini.

> **Dk. Kashenge anasema takwimu za Benki Kuu ya Tanzania (BoT), zinaonyesha upatikanaji mafuta ya kula nchini ni asilimia 40 na asilimia 60 ni mafuta kutoka nje ya nchi.**

Anasema, ni aina ya mageuzi yatakayosaidia hata baada ya kati ya miaka miwili hadi mitatu, uzalishaji utaongezeka na kusaidia kushuka bei ya mafuta ya alizeti kwa walaji, ambayo kwa sasa ni kati ya Sh, 19,000 hadi Sh. 20,000 kwa lita tano.

Mkuu huyo wa Wakala wa Mbegu, anaelekeza pongezi kwa serikali kuwanunulia matrekta matatu mwaka jana, akitaja zikiwa na nyenzo za kunyunyizia dawa mbili, pia upandaji wote zikiwa na thamani ya Sh. bilioni moja.

Hivyo, anasema ili waweze kufanya kazi vizuri, wanahitaji jumla ya matrekta 19 na zana zake na kwa sasa wana matrekta sita pekee.

**NAIBU WAZIRI**

Naibu Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba, anasema suala la mazao ya kimkakati nchini, litasaidia upatikanaji alizeti na kuweza kuendesha viwanda vya ndani kwa mwaka mzima, hivyo kudumisha na kutanua ajira kwa wananchi.

Anasema, uzalishaji mdogo wa la alizeti uliopo sasa nchini unavifanya viwanda vya ndani kuendeshwa kwa nusu mwaka, tofauti na malengo yaliyopo, hali inayotishia uwepo viwanda uchumi wa nchi na maslahi ya vijana kitaifa.

Mgumba anawashauri wakulima waendelee kufuata ushauri wa kitaalamu wa kilimo cha alizeti, ili kuweza kupata mavuno mengi kwa msimu na kutosheleza mahitaji ya ndani na pengine nje ya nchi.

Anasema serikali imeona mazao hayo, zikiwemo alizeti na michikichi kuwa ndio pekee yanavyoweza kusaidia upatikanaji wa mafuta ya kula kwa wingi nchini, hata taifa likaachana na ununuzi ya mafuta kutoka nje ya nchi, jambo litakalosaidia kubakiza fedha za ndani na kukuza uchumi.

Mwaka 2018, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kebwe Steven Kebwe, alitoa agizo la siku 14 kuzuia wananchi kuingia kwenye maeneo ya Wakala wa Mbegu, baada ya kuwapo uvamizi



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mbegu Tanzania, Dk. Sophia Kashenge, akimuonyesha Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, mfuko wa mbegu za alizeti zinazozalishwa na ASA, wakati waziri huyo alipofanya ziara ya kikazi mkoani Morogoro

# Taharuki corona sokoni na tetesi zake mtandaoni, bidhaa zimedoda

## • Wapo wa butwaa, wengine waamua

**Na Jenifer Gilla**

DUH! hii corona sasa inakoelekea itatulaza na njaa," Ramadhani Mikidadi, maarufu kama Rama, anajikuta anaropoka kwa sauti ya juu , huku akiikodolea macho simu yake katika mtazamo wa kutoamini anachokisoma.

"Kuna nini tena?" ni swali lililobeba mshangao unaohamia kwa jirani yake, anayedaka butwaa hilo pasipo kujua undani wa kilichojiri na anaamua kupiga hatua kumsogelea Rama, ili aelewe kinachomsibu.

Hapo naye, jirani huyo baada ya kupata jibu, ghafla anaendeleza kwa mtindo uleule wa kilichomtokea Rama, akitahamaki kwa kauli "kweli aisee! Kwa hali hii, tutafunga biashara."

Hicho ndicho kilichotawala ndani ya dakika kadhaa, hali ya taharuki inatawala soko la mitumba Mwenge, jijini Dar es Salaam, hata ndani ya muda mfupi kunatekwa na makundi ya watu wanaoonekana wakijadili jambo hilo.

Kisa kikuu hapo ni ujumbe unaosambaa kwenye mtandao wa 'whatsap' uliowafungulia mada ya kuumiza kichwa juu ya hatma ya mwenendo wa biashara yao.

Ujumbe unawasilishwa kwa sauti inayotahadharisha watu kutonunua nguo za mtumba kwa kipindi kilichopo cha mlipuko wa ugonjwa corona, kwa kuwa 'mabelo' ya nguo za mtumba walizotumia wagonjwa wa corona nchini China, yanaletwa barani Afrika.

**MSHITUKO ULIVYOWAGUSA**

Ramadhani Mikidadi, maarufu kama Rama ni mfanyabiashara wa bidhaa za mtumba ya midoli ya watoto sokoni hapo, anayesema tangu kuenea maambukizi ya ugonjwa wa corona, mauzo ya bidhaa zake yameshuka kutokana na mzunguko kuwa mdogo, lakini anahofu ujumbe huu unaozunguka unaweza kuua kabisa biashara yake.

"Ujumbe huu umenishtua, kwa kuwa mimi nategemea wateja wa nguo za mtumba ndio wanunue na kwangu. Sasa kutokana na huu ujumbe kutembea, ni dhahiri kuwa wateja wa nguo za mtumba hawatokuja tena huku," anasema Rama

Mfanyabiashara huyo analalamika tangu kuenea kwa ugonjwa wa corona, bidhaa zake zimedoda, kutokana na wateja kubaki majumbani wakiepuka msongamano uliopo.

"Biashara imeyumba sana! Zamani nilikuwa nikikusanya hadi Sh. 100,000 kwa siku, ila kwa sasa nikipata sana ni Sh. 10,000. Hii yote ni kwa sababu mzunguko wa watu umepungua," analalamika Rama.

Mfanyabiashara mwenzake wa nguo za mtumba, maarufu kwa jina la Obo, anasema nguo za mtumba zimeshuka thamani, kwa sababu watu hawavutiwi kuzinunua, kwa kuwa hakuna tena shughuli zinazomlazimu mtu kufika mahali hapo, akanunua nguo hizo.

"Unajua nguo za mitumba zinaendana na 'occasion' (shughuli maalum), ambayo kwa sasa serikali imezuia kupisha 'hili gonjwa' la corona, kwa hiyo watu hawana sababu ya kuja kununua nguo,: anaelezea nafasi yake.



Wauza mitumba wa soko la Mwenge, wakiendelea na kazi katika zama za Corona. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **"Ujumbe huu umenishtua, kwa kuwa mimi nategemea wateja wa nguo za mtumba ndio wanunue na kwangu.**

Obi ambaye kabla ya kuzuka janga la corona, alikuwa ana mapato ya mauzo kati ya Sh. 65000 hadi 100,000 kwa siku, kwa sasa analalamika kuambulia Sh. 20,000 kwa siku, huku akielekeza kiulizo dhidi ya ujumbe unasambaa, kumuweka hatari ya njia panda, asimudu kuuza chochote kabisa kwa siku.

Japo idadi kubwa ya wafanyabiashara wanalalamika kudorora mauzo, kwa upande wa pili wa shilingi, wapo wenye mtazamo kwamba bado hawajaguswa sana na athari hizo.

Grace Michael, mfanyabiashara wa pochi na viatu vya mitumba, anasema kwa upande wake biashara bado si mbaya, kwa sababu hategemei sana wafanyabiashara wa kupita, bali wa mtandaoni.

"Mimi bidhaa zangu nauza sana mtandaoni ndugu mwandishi. Hapa nimeegesha tu, bidhaa zangu napiga picha, naweka 'insta' (instagram), mteja akipenda analipia, nampa bodaboda anampelekea alipo" anafafanua Grace, katika kauli ya kujiamini katika ujasiriamali.

Zuberi Kafumula, pia anaangukia aliko Grace, ingawa yeye ana banda la biashara katika eneo hilo, lakini amejikita zaidi kuuza bidhaa kwenye minada ya sokoni, kwa hiyo mauzo yake hayajashuka.

Anasema, tangu wahamishiwe katika soko jipya, wateja walikuwa hawafiki mahali hapo, hivyo alijiongeza kwa kubuni mbinu ya kuuza bidhaa zake kwenye minada, hali inayomsaidia asitegemee sana kuuza biashara zake katika soko hilo la Mwenge pekee yake.

**WENGINE WAKIMBIA**

Bado inabainika, kombora la ugonjwa corona ni zito, kwani wapo wafanyabiashara waliolazimika kupakimbia Mwenge na wengine wameacha kabisa.

Walichoamua kwa muda sasa, wameenda kutafuta biashara sehemu nyinginezo, wakiamini kuna nafuu ya kibiashara.

Mmoja wao anajitamulisha kwa moja la Ismaili, aliyelazimika kuhama eneo la biashara Mwenge na kwenda Tandika kujishikiza, akipanga kurudi baadaye, pindi biashara 'itakapochangamka' katika sura ya zamani walioizoea.

"Unajua tangu tuhamie soko jipya, biashara ni ngumu kutokana na kwamba wateja wengi hawajakuzoea huku. Sasa tangu kuwepo huu mlipuko, hali imekuwa mbaya zaidi.

"Sikufichi dada yangu, ilifika mahali nikawa sipati hata shilingi wiki nzima, nikaona nijiongeze kutafuta sehemu iliyochangamka ili niokoteokote, nitarudi hali ikikaa sawa," anasema Ismail.

Nipashe imegundua baadhi ya wafanyabiashara wenye biashara zaidi ya moja, wamelazimika kufunga biashara sizizo na wateja ili kupunguza hasara.

Dominick, maarufu kwa jina Domy, aliyekuwa na biashara mbili anasema, alilazimika kufunga biashara ya midoli na akabaki na viatu, kwa kuwa ndio ina wateja kwa sasa.

**HALI YA UGONJWA**

Taarifa ya Wizara ya Afya, Maendeleo, Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inafafanua kwamba, virusi vya corona nchini Tanzania, idadi ya watu waliothibitika kuwa na maambukizi ya ugomjwa huo mpaka jana asubuhi wamefikia 94, huku wagonjwa wanne walifariki na 11 wamepona.

Serikali ilishachukua hatua ya kuzuia mikusanyiko ya watu kama kwenye matamasha ya muziki na mikutano ya hadhara na imekuwa ikihamasisha watu kunawa mikono na kutumia vitakasa mikono, ili kuepuka kuambukiza na kuvisambaza virusi hivyo.



Mandhari ya shughuli za biashara ndogo, eneo la Mwenge kabla ya mabadiliko hivi karibuni.





# Kanisa latoa vifaa tiba mil. 50/- kujikinga corona

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Kati (DCT), Dk. Dickson Chilongani, amempongeza Rais Dk. John Magufuli, kwa ujasiri aliouonyesha kwa kuruhusu nyumba za ibada kuendelea na ratiba zao wakati huu dunia ikiwa katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu corona (Covid-19).

Dk. Chilongani alisema, ujasiri ulioonyeshwa na Rais Magufuli ni kukataa kuiga mataifa ya nje yalipozuia ibada kuendelea kufanyika, lakini yeye alimtegemea Mungu na kuwataka Watanzania waombe sana ili tatizo hili liondoke haraka.

Akizungumza jana katika makao makuu ya kanisa hilo jijini hapa, alipokuwa anakabidhi vifaa tiba vya kuzuia maambukizi ya Corona kwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobasi Katambi, Askofu Chilongani alisema, pamoja na kufuata masharti ya kujikinga, Mungu naye ana nafasi yake.

"Watanzania, Rais wetu Dk. Magufuli ameonyesha ujasiri mkubwa, kwa kuwa licha ya mataifa ya Ulaya kufunga nyumba za ibada kutokana na corona, yeye alisimama katika imani yake na kutaka nyumba za ibada ziendelee kama kawaida," alisema Dk. Chilongani.

Kadhalika, Askofu Chilongani aliwataka Watanzania wasifanye makosa katika Uchaguzi Mkuu wa Urais mwaka huu, wachague kiongozi ambaye ana hofu ya Mungu, kitendo kilichoonyeshwa na Rais Magufuli katika kipindi hiki dunia imetaharuki kutokana na corona, imeonyesha wazi kuna kiongozi ambaye anaongozwa na Mungu.

"Sisi watu wa kiroho tunaelewa hata kama tutatumia vifaa tiba vya kuzuia maambukizi, lakini bila Mungu hatuwezi kutokana hapa tulipo, kama ni utajiri au wingi wa vifaa, mbona mataifa ya Ulaya wameshindwa kuudhibiti na wanakufa kila siku kwa maelfu ya watu?" Alihoji.

Askofu Chilongani alisema Rais Magufuli alimtanguliza Mungu katika mapambano dhidi ya ugonjwa huu, na wao kama kanisa wanamuunga mkono Rais kwa maombi, pia kwa kutoa vifaa vya kujikinga na maambukizi ya virusi hivyo.

"Yesu alipoondoka hapa duniani alisisitiza upendo, bila kujali itikadi au dini ya mtu, ndio maana sisi tumeamua kutimiza wajibu wetu katika kutoa msaada wa vifaa hivyo katika wilaya tatu, Dodoma, Bahi na Chamwino", alisema Askofu Dk. Chilongani.

Pia, alisema wamefanikiwa kukusanya Sh. milioni 50 walizonunua vifaa hivyo ambavyo watakabidhi katika ofisi za wakuu wa wilaya.

Akipokea msaada huo, Katambi alisema kilichofanywa na Askofu huyo na waumini wake ni jambo la kuigwa kwa kuwa ni mfano mzuri katika jamii, licha ya kuwa kiongozi wa kiroho lakini yanapotokea majanga kama hayo wanatoa msaada pia.

Katambi alisema kanisa hilo limeonyesha utashi na upendo kwa watu kwa kuunga mkono jitihada za serikali katika mapambano dhidi ya corona.

"Nashukuru sana Askofu na waumini wako kwa kitendo cha kutoa msaada huu.

Pia tunashukuru kwa maombi yenu viongozi wa dini, tunaamini kufuatia ibada zilizoruhusiwa na serikali Mungu atanyoosha mkono wake na kutuepusha na janga hili ambalo dunia nzima inahangaika kulitokomeza," alisema.

Katambi alisema vita dhidi ya corona inapigana na mataifa makubwa duniani na wanaangamia, haya ni kama mafunzo, suala la toba linatakiwa ili Mungu awarehemu.

Alisema serikali imefanya mambo mengi mazuri na makubwa, lakini hata katika mapambano dhidi ya corona imekuwa mstari wa mbele kutoa elimu na huduma nzuri kwa waathirika na washukiwa.



Kinamama wakifanya kibarua cha kukusanya mchanga kwa ajili ya ujenzi ili kujipatia kipato cha siku, katika barabara ya Mbeya, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakazi Dodoma wasisitizwa kuchukua tahadhari

**Na Renatha Msungu,**
dodoma

WAKATI dunia ikiendelea kupambana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Corona-19), wakazi Jiji la Dodoma wameshauriwa kuendelea kuchukua tahadhari kwa kufuta maelekezo yanatolewa na Wizara ya Afya.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa Matekelezo kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya afya (NHIF), Bakari Said, wakati akizungumza kwenye mahojiano na vyombo vya habari jijini hapa.

Alisema wakati wote wananchi wapaswa kufuata maelekezo yanayotolewa ya kujikinga na ugonjwa huo ambao kwa sasa umekuwa ni janga kubwa ulimwenguni na endapo watu wakizembea yale ambayo wanaelekezwa changamoto itakuwa kubwa zaidi. Pia alisema mfuko huo umefanikiwa kutoa kadi kwa wananchama wake ambao umewasaidia katika kukabiliana na changamoto mbalimbali, lakini yanapojitokeza magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, ebola, corona huwa na utaratibu wake.

Said alisema NHIF, ikiwa kama mdau kwenye sekta ya afya wameendelea kuwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari zinazotakiwa ili kuhakikisha maambukizi hayaendelei.

Alitoa msisitizo kwa wananchi kujiunga na mfuko huo ili kuwa na uhakika wa matibabu tatizo linapojitokeza na wasisubiri lijitokeze ndipo wajiunge huku akisema kuwa Watanzania bado wananafasi ya kupata taarifa mbalimbali zinazohusiana na bima ya afya kwa kupitia kitengo maalumu kilichopo katika ofisi za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kinachoitwa kitengo cha huduma kwa wateja.

# Watakiwa kuwa wabunifu kuongeza mitaji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, ameutaka Umoja wa Wafanyabiashara Minadani (Uwabimido) kuacha kufanya kazi kwa mazoea, ili waweze kukuza mitaji yao.

Ushauri huo aliutoa alipokuwa akizungumza na viongozi wa umoja huo wa wafanyabiashara wa minadani Mkoa wa Dodoma, kwenye ofisi na makao makuu ya umoja zilizopo jijini hapa.

Yuna alisema ili kwenda na kasi ya biashara zao wanatakiwa kutofanya biashara zao kwa mazoea, na kuhakikisha wanafikia malengo ya kuinua mitaji yao kukuza kiuchumi na hatimaye kuwa wafanyabiashara wakubwa.

Aliwataka kuepukana na migogoro isiyo na tija ambayo mara nyingi inarudisha nyuma maendeleo yao.

Hata hivyo, alisema wafanyabiashara wote wa minadani wanatakiwa kuwa katika eneo moja ambalo litakuwa linajulikana na kuondokana na kukaa kwenye maeneo yasiyo rasmi ambayo yanaweza kusababisha ajali kwa mali zao na wateja.

Katika hatua nyingine, Yuna aliwataka kuhakikisha wanafanya kazi zao kwa kushirikiana na halmashauri husika, ikiwa ni pamoja na kufuata maelekezo na kanuni wanazoelekezwa ili waweze kufanya biashara kwa uhuru na ufanisi.

"Ili umoja wenu uweze kufanya biashara kwa uhuru na ufanisi, mnatakiwa kufuata maelekezo yanayotolewa na halmashauri husika huko mnakofanyia biashara zetu, tumieni umoja wenu kushirikiana na halmashauri na hapo mtajikuta mkifanya kwa uhuru zaidi," alisema.

Pia alisema, ili biashara iweze kustawi, wafanyabiashara hao wanatakiwa kufanya kwa njia ya utulivu, amani pamoja na kuzitii mamlaka kwa kufuata maelekezo wanayopewa badala ya kuwa na malumbano na mamlaka husika.

Naye Mwenyekiti wa wafanyabiashara hao minadani katika mkoa wa Dodoma, Jeremia Magawa, alisema malengo na maazimio ya kuwa na ofisi kuu ni kutokana na kuitikia kauli ya halmashauri ya jiji ya kuliweka jiji katika mpango mzuri.

Alisema hapo awali walikuwa wanazagaa maeneo mbalimbali bila mpangilio, hali iliyokuwa ikionyesha kuwa ni wachafunzi na waharibifu kutokana na kutokuwa na ofisi ambayo itawafanya watulie.

Hata hivyo, Mwenyekiti huyo ameziomba halmashauri za mkoa wa Dodoma kuhakikisha wafanyabiashara wa minadani wanaondolewa kwenye maeneo yasiyo rasmi ili kuondoa misongamano inayoweza kuhatarisha usalama na kuwapo kwa uchafuzi wa mazingira.

"Tunaziomba mamlaka husika ikiwamo jiji na halmashauri za wilaya, mamlaka husika huhakikisha wanawaondoa wafanyabiashara waendao minadani ambao waliokataa kuondoka kwenye maeneo yasiyo rasmi na kusababisha msongamano usiokuwa walazima," alisema.





## Siri utulivu Tanzania, Malawi yafichuliwa

**Na Grace Mwakalinga,**
KYELA

IMEELEZWA kuwa, utulivu wa kisiasa na kijamii katika nchi za Tanzania na Malawi unatokana na uboreshaji wa huduma ambazo zinasababisha wananchi wa mataifa hayo kupata mahitaji yao bila usumbufu.

Kadhalika, kuzitumia fursa zinazowekwa na serikali kwa ajili ya kuendesha maisha na kukuza uchumi wa mataifa yao.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert chalamila, wakati akitembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa kituo cha pamoja cha forodha baina ya Tanzania na Malawi kinachojengwa katika mpaka wa Kasumulu wilayani Kyela.

Alisema kutengemaa kwa siasa kati ya nchi hizo mbili ni mipango mathubuti uliowekwa na viongozi kwa kuhakikisha wanaboresha huduma nyingine muhimu ikiwamo ujenzi wa kituo cha pamoja cha forodha ambazo kitakuza uchumi.

"Lengo letu ni kuhakikisha kituo hiki cha pamoja cha forodha kinakuza uchumi kwa nchi zote mbili hasa kwenye masuala ya kodi na kiuhamiaji na kukuza mapato lakini kuboresha maisha ya wananchi kupitia biashara zao," alisema Chalamila.

Mwakilishi wa Tanroads, mkoani humo, Mhandisi John Mahenge, alisema mradi wa ujenzi wa kituo cha pamoja cha forodha kati ya Tanzania na Malawi kwa upande wa Tanzania unatekelezwa na Serikali kupitia Tanroads kwa zaidi ya Sh. bilioni 26.

Alisema ujenzi umefikia asilimia 23 na hadi kukamilika unatakiwa kufikia asilimia 50, kazi bado inaendelea licha ya changamoto ya hali ya hewa, huku akidai forodha hiyo itasaidia kupunguza msongamano na kuongeza mapato ya serikali katika mpaka huo.

Baadhi ya wananchi wa Tanzania na Malawi , Grace Miyombe na Fred Samson, walisema mradi huo ni mzuri kwa vile utaboresha mazingira yao kazi hasa kwa wajasiriamali waishio jirani na mpaka huo.

# Msako wa nyumba kwa nyumba kukagua vifaa vya hadhari corona

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, amesema wanao mpango wa kufanya msako wa nyumba kwa nyumba ili kuhakikisha kila kaya ina ndoo za maji, sabuni au vitakasa mikono katika kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema wameweka nguvu kubwa kutoa elimu kwenye maeneo yenye mikusanyiko ikiwamo sokoni na vituo vya mabasi, sasa wanahamia kwenye kaya kutoa elimu hiyo pia.

Ntinika alitoa kauli hiyo jana wakati akitoa elimu ya kujikinga na ugonjwa ya Covid-19 katika maeneo ya kituo cha daladala cha Kabwe, soko la Soweto, Uyole na Igawilo. "Tunaendelea kutoa elimu kwa kila mwananchi hususani walioko kwenye makundi juu ya umuhimu wa kunawa mikono mara kwa mara, sio fasheni bali ni kinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona, maana wako baadhi ya watu wanabeza jambo hili," alisema Ntinika.

Alisema kampeni ya nyumba kwa nyumba kutoa elimu ya kujikinga na ugonjwa wa Covid-19 kwa kuhimiza unawaji wa mikono mara kwa mara itasaidia kulinda watoto. Baadhi ya wananchi jijini humo, wamelalamikia gharama kubwa ya ndoo kutoka Sh. 2,000 ya awali hadi Sh.5,000 kwa sababu na kuiomba serikali kudhibiti upandaji holela wa vifaa ya kunawia mikono ili kila mtu amudu gharama na kujikinga na ugonjwa huo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, Hassan Mkwawa, alisema kuwa, madereva Bajaj hawajachukua tahadhari zozote za kukabiliana na ugonjwa wa Covid-19 ikiwamo kuweka ndoo na sabuni kwenye bajaji zao.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipokuwa akipokea vifaa vya kisasa vya kunawia mikono vilivyobuniwa na wanafunzi wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Must), aliagiza kila ofisi ya umma lazima inunue kifaa hicho na atakayekaidi apewe taarifa.

Alisema jitihada zote hizo ni katika kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona kwa kuhakikisha kila sehemu ya kutolea huduma kunakuwa na vifaa vya kunawia mikono.



Muonekano wa eneo la Igawa, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, baada ya kukamilika kwa mradi wa upanuzi wa barabara kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam), na kuwekwa taa zinazotumia nishati ya jua, katika eneo hilo ambalo mradi huo umeisha. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wajane Kyela waboreshewa makazi

**Na Grace Mwakalinga,**
KYELA

JUMLA ya wajane sita wa Kata ya Mwaya katika Halmshauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, wamenufaika na msaada wa kuboreshewa makazi uliotolewa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la Vision Trust Tanzania.

Shirika hilo linajishughulisha na kuhudumia watoto yatima, wajane na wagane.

Akizungumza na Nipashe jana, mmoja wa wajane hao, Editha Makula (70), anayeishi na wajukuu zake saba alioachiwa na watoto wake watatu baada ya kufariki, alisema awali alikuwa anaishi kwenye nyumba ya udongo iliyoezekwa kwa nyasi na kwamba msimu wa mvua walishindwa kulala.

Alisema baada ya kuona mazingira anayoishi Shirika la Vision liliamua kumjengea mjane huyo nyumba ya kisasa ili aondokane na adha aliyokuwa akiipata kipindi cha mvua.

"Sikuwahi kuwaza kama ntakuja kuishi kwenye nyumba nzuri kama hii, maana sina uwezo wowote wa kifedha, watoto wangu niliokuwa nawategemea wote walifariki na kuniachia wajukuu saba ambao nawalea," alisema Editha.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Mchungaji Clement Mwaitebele, alisema jumla ya Sh. milioni 40 zilitumika kwenye ujenzi wa nyumba sita ambazo zilijengwa katika Kata ya Mwaya.

Alisema walishawishika kuwajengea wajane hao nyumba baada ya kuona wakiishi kwenye nyumba zenye usalama mdogo, alidai nyumba hizo zilikuwa zimejengwa kwa miazi na kuezekwa kwa nyasi.

"Mwaka 2010 ndipo tulianza kuwajengea wajane nyumba bora za kuishi na tulikuwa tunajenga kwa awamu kadri pesa zinavyopatikana, tuliona nyumba ni kipaumbele cha kwanza kwao kwa sababu ya hali duni walionayo na kushindwa kuhudumia vyema watoto yatima", alisema Mchungaji Mwaitebele.

Alisema wameboresha makazi kwa wajane wa Kata ya Mwaya pekee, lakini uhitaji ni mkubwa hivyo wana malengo ya kuhudumia wajane wa wilaya nzima ya Kyela.

Aliongeza kuwa, jumla ya watoto 300 ambao ni yatima katika Kata ya Mwaya wa shule za msingi na sekondari wamepatiwa msaada wa sare za shule, madaftari, viatu mashuka na kupatiwa uji kila siku ya jumamosi.

Alisema watoto hao walikuwa wanakosa mahitaji hayo muhimu kutokana na familia zao kuwa duni, na kwamba wengi wa watoto hao wanaishi na bibi zao.

Aliiomba Serikali kuunga mkono juhudi hizo ili wajane na watoto yatima waishi maisha ya furaha kama ilivyo kwa wengine na kwamba uhitaji bado ni mkubwa.





# RC awapa masheha jukumu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi Unguja, Hassan Khatib Hassan, amewataka masheha wa mkoa huo kusimamia kwa karibu vikundi vya ulinzi shirikishi ili kuimarisha ustawi wa jamii wakati taifa likipambana na maambukizi ya corona.

Akizungumza kwa wakati tofauti katika vikao vilichowashirikisha viongozi wa wilaya, manispaa na Jeshi la Polisi, Hassan alisema vikundi vya ulinzi shirikishi vinapaswa kuendesha shughuli zao vizuri kama ilivyo azma ya serikali.

Alisema serikali imeanzisha vikundi hivyo kwa nia nzuri ya kuwashirikisha wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kulinda usalama wao na mali zao, hivyo sio busara kuona wanatumia vibaya nafasi hiyo.

"Serikali imekuwa na dhamira njema kuruhusu kuanzisha ulinzi shirikishi kwa vile vikosi vyetu vya ulinzi pekee visingetosheleza kusimamia usalama katika maeneo yote na muda wote," alisema Hassan.

Aidha Mkuu huyo wa mkoa aliwataka viongozi hao kushirikiana kuandaa utaratibu maalum utakaohusisha upatikanaji wa sare na vitambulisho vya kuwatambua pamoja na kuwapatia mafunzo ya kukabiliana na vitendo vya uhalifu.

Akizungumzia kuhusu kukabiliana na maambukizi ya maradhi ya corona, Mkuu huyo wa mkoa aliwataka masheha kupita nyumba kwa nyumba kutoa elimu juu ya madhara hayo huku akiwataka kutoa taarifa za wageni wanaoingia katika shehia zao.

Katika hatua nyingine, Hassan aliwataka viongozi wa mabaraza ya Manispaa mkoani humo kushirikiana na Jeshi la Polisi kutambua vituo vya vyombo vya moto ikiwamo pikipiki umaarufu kama bodaboda zilizomo katika manispaa zao ili kupunguza vitendo vya uhalifu na ajali za mara kwa mara.

Akizungumza katika mkutano huo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Kamishna Msaidizi Awadh Juma Ali, alisema Jeshi la Polisi litachukulia hatua baadhi ya vikundi vya watu vinavyojihusisha na matendo ya uhalifu katika mkoa huo.

Aidha aliwaomba masheha kushirikiana na Jeshi hilo kubaini vikundi vinavyojishughulisha na masuala ya uhalifu katika maeneo yao ili vidhibitiwe kwa kuchukuliwa hatua.

Alisema Jeshi la Polisi litahakikisha linasimamia kwa karibu maelekezo, miongozo na maagizo ya serikali kuu kuhusu kutokuwapo kwa mikusanyiko isiyokuwa ya lazima na kuwataka wananchi kufuata maelekezo hayo sambamba na kutii sheria bila ya shuruti.

Wakizungumza baada ya mkutano huo, baadhi ya viongozi walioshiriki vikao hivyo waliahidi kuyafanyia kazi maagizo na maelekezo yaliyotolewa na kuwataka wananchi kutoa ushirikiano ili kuhakikisha mapambano ya maambukizi ya corona yanafanikiwa.



Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa Wilaya ya Magharibi 'B', Unguja, Ali Abdallah Natepe (kushoto), akizungumza na vijana ambao wapo kijiweni katika Mtaa wa Mwanakwerekwe jana. Haya hivyo, serikali imekataza watu kukaa vikundi ili kuchukua tahadhari ya maambukizi ya virusi vya corona. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ulipaji pensheni kwa wazee bila msongamano waja

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Fatma Gharib Bilali, amesema serikali itaendelea kutoa pensheni jamii kwa wazee katika utaratibu unaofaa ili kuondoa msongamano.

Akizungumza na wazee alipotembelea ugawaji wa pensheni jamii katika kituo cha Shule ya Kiembe Samaki, alisema utaratibu huo unazingatia maelezo yanayotolewa na Wizara ya Afya kwa lengo la kuepukana na maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema ikiwa leo ni siku ya kwanza kutoa pensheni hiyo tangu kuzuka kwa ugonjwa wa corona visiwani Zanzibar, kila mmoja anawajibu wa kuchukua tahadhari juu ya kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema hawatasajili wazee wapya kutokana na changamoto iliyopo, hivyo wataendelea kutoa pensheni hiyo kwa wazee waliosajiliwa. Kwa upande wao wazee waliopokea pensheni hiyo, walisema utaratibu wa kunawa mikono kabla ya kupokea pensheni hiyo ni mzuri, na kuiomba serikali wauendeleze ili kunusu afya zao.

Pensheni jamii hutolewa kila mwezi kwa wazee waliofikia miaka 70 visiwani Zanzibar.

# Mfumo wa kielektroniki waiva kuwafuatilia madereva wakaidi

**Na Rahma Suleimn,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar inakusudia kuanzisha mfumo wa kielektroniki ili kuvitambua vyombo vya moto vinavyotembea barabarani kwa lengo la kuvifuatilia na kubaini madereva wanaokiuka sheria.

Akiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi ya Mwaka 2019/2020 kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasilino na Usafirishaji, Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Sira Ubwa Mamboya, alisema katika kutekeleza suala hilo, serikali imeanza kutumia mfumo wa kamera za CCTV zilizowekwa kwa matumizi ya mji salama ili kubaini makosa ya usalama barabarani.

Aidha alisema Idara ya Usafiri na Leseni inazipitia kanuni mbalimbali za usalama barabarani na kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua za kisheria madereva wote watakaobainika kufanya makosa ya barabarani kwa lengo la kuwadhibiti na kunusuru maisha ya wananchi na mali zao.

Dk. Sira alieleza Serikali inaandaa utaratibu wa faini za papo kwa papo ili kuharakisha hukumu na adhabu kwa madereva wazembe na wanaokwenda kinyume cha sheria za usalama barabarani.

"Serikali inaandaa utaratibu wa kuwatoza faini watakaobainika kufanya makosa ya barabarani kwa njia za kielektroniki ili kukusanya fedha hizo hapo hapo (barabarani) au kupitia benki kwa atakaebainika kufanya makosa," alisema.

Alieleza kuwa rasimu ya kanuni hizo za adhabu ya papo kwa papo imekamilika na kwa sasa ipo wizarani kwa mapitio.

Akichangia hoja hiyo, Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni, Rashid Makame Shamsi, aliishauri Wizara hiyo kuwashirikisha wadau wote wakati wa utungaji wa kanuni hizo ili kuondoa malalamiko wakati wa utekelezaji wake.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

### TANGAZO LA KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAHIM SALIM MOLLEL** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 395 CXJ TOYOTA VEROSSA Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: ARU/ARU/RB/303116/2020

157053

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

KINGLION INVESTMENT COMPANY LIMITED anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 219 CMV.
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: MBE/MBE/RB/301377/2020.

157052

### ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPLIES T. LTD &COURT BROKER

**MNADA WA HADHARA**

KWA AMRI TULIYOPEWA NA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA DODOMA MJINI TUTAUZA KIWANJA KILICHOPO MJIMPYA PLOT NO. 11 BLOCK 16 .TAREHE 15/05/2020 SAA 4:00 ASUBUHI.

KWA MAWASILIANO ZAIDI. 0713913150.

157049

### TANGAZO,

**Mimi Said Ahmad Simba** natangaza kupotelewa (Offer) ya Kiwanja Namba 224 Kitalu Z kilichopo katika eneo la Ibinzamata, Manispaa ya Shinyanga.

Nimeripoti katika kituo cha Polisi cha mjini Shinyanga na kupewa kumbukumbu Namba ya malipo 9910812402584 ya tarehe 15/04/2020.

Kwa yeyote atakayeikota aipeleke katika Kituo cha Polisi kilichopo karibu naye au wasiliana kwa namba.

**0767-499131.**
**0787-799131.**

157050

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**DAVIDI THADEO MUSHONGOLE** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya **FEKON** yenye rangi nyekundu. Yenye namba ya usajili **MC 158 CEH.** Chassis namba **LDAPAJOB4KGB00946.** Engine namba **157FM1-2*19F00946.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **MWA/NY/RB/313062/2020.**

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HEZRON GIDION WAILES** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 376 BPA.** Yeyote atakayeiona atoe taareifa kituo cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/317895/2020.**

*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la Nipashe*

*kila siku Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# EU: Hali Msumbiji inatia wasiwasi

**Maputo,** Msumbiji

UMOJA wa Ulaya (EU), umesema una wasiwasi mkubwa na kuongezeka kwa ghasia kaskazini mwa Msumbiji, na kuvurugika kwa hali ya kibinadamu katika eneo hilo.

Katika taarifa iliyoitoa jana, EU imesema hali ya usalama katika mkoa wa Cabo Delgado ulio kaskazini mwa nchi hiyo imezorota sana wiki za hivi karibuni, na kuyataja mashambulizi ambayo yamekuwa yakiongezeka.

Mkoa huo unayo miradi ya uchimbaji wa gesi yenye thamani ya mabilioni ya dola, inayoendeshwa na kampuni kubwa za kimataifa, ikiwamo Total ya Ufaransa.

Mwezi uliopita wanamgambo waliyakamata majengo ya serikali katika mkoa huo na kupandisha bendera ya kundi linalojiita Dola la Kiislamu.

Taarifa ya EU ilieleza kuwa mipango madhubuti inahitajika kuishughulikia hali ya sasa katika mkoa wa Cabo Delgado, ili kuwalinda wananchi na kufanya uchunguzi utakaohakikisha kuwa wanaohusika katika ghasia hizo wanafikishwa mahakamani.

Ilieleza kuwa, kuwapo wa vurugu kumesababisha idadi kubwa ya wakazi kuyakimbia makazi yao.

Kwa mujibu wa Askofu wa Dayosisi ya Pema, Dom Luiz Fernando Lisboa, tayari watu 200,000 wameyakimbia makazi yao kutokana na ghasia hizo, nalo Shirika la Madaktari wasio na Mpaka (MSF) limesema wengine 700 wamepoteza maisha.

Aidha, EU umeitaka serikali ya Msumbiji kuchunguza haraka kisa cha kutoweka kwa mwandishi wa habari wa redio ya kijamii ya Palma wiki iliyopita. Mwandishi huyo, Abu Mbaruko alitoweka alipokuwa njiani akirejea nyumbani kutoka kazini na hadi sasa hajulikani alipo.

Aprili 7, mwaka huu, Mbaruko aliwatumia wenzake ujumbe wa maandishi akiwaarifu kuwa alikuwa amezingirwa na wanajeshi, na tangu hapo, hajaweza kupokea simu anazopigiwa.

Licha ya ahadi iliyotolewa na Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi, vyombo vya usalama vya Msumbiji vinavyosaidiwa na mashirika binafsi ya usalama ya kimataifa, havijaweza kuyasimisha mashambulizi katika mkoa huo.

Umoja wa Ulaya katika taarifa yake umeahidi kuisaidia Msumbiji katika juhudi zake za kuyasambaratisha makundi yanayovuruga usalama.

Hata hivyo, kamanda mkuu wa polisi wa Msumbiji, Bernardino Rafael, amekanusha habari za makundi hayo kuyadhibiti maeneo ya kaskazini mwa Msumbiji, akisema kilichopo ni mashambulizi madogo ya wahalifu katika baadhi ya sehemu.

Kamanda huyo lakini amekiri kuwa hali ya hofu imetanda katika baadhi ya maeneo ya mbali na miradi ya kuchimba gesi, kama vile Mocimboa da Praia.

DW



Wananchi wa Mkoa wa Cabo Delgado uliopo Kaskazini mwa Msumbiji, wakiwa katika maandamano. **PICHA: DW**

# Vifo vya corona Marekani vyafikia 30,800

**WASHINGTON,** Marekani

HADI kufikia jana jioni, idadi ya watu waliofariki kutokana na ugonjwa wa virusi vya corona nchini Marekani ilikuwa 30,800, huku zaidi ya 638,000 wakiugua.

Akizungumza na waandishi wa habari, Rais wa nchi hiyo, Donald Trump alisema: "Takwimu za kitaifa zinaashiria, tumepita kilele cha maambukizi mapya ya virus vya corona, ni matumaini yangu tutaendelea hivyo, na tutaendelea kupiga hatua zaidi".

Alipoulizwa kama ni kweli Marekani ina idadi kubwa ya watu 136,908, waliofariki kutokana na ugonjwa huo kote duniani, Rais Trump alilaumu baadhi ya mataifa kwa kutoa taarifa za uongo kuhusu idadi ya vifo.

Rais Trump alisema Marekani inachunguza madai kuwa virusi vya corona vilikuzwa ndani ya maabara mjini Wuhan na kwamba chanzo chake sio soko la mji huo.

Vyombo vya habari nchini Marekani vimeripoti kuwa ubalozi wa nchi hiyo mjini Beijing unahoji usalama wa maabara mbili zilizopo Wuhan.

Hata hivyo, siku ya Jumanne, Jenerali Mark Milley, mwenyekiti wa pamoja wa wakuu watumishi wa umma, alisema idara ya ujasusi wa Marekani inaamini huenda janga la corona siyo janga la kawaida.

Utawala wa Rais Trump uliwahi kusema kuwa Mei mosi ndiyo tarehe ambayo taifa hilo huenda likarejea hali yake ya kawaida, alisema baadhi ya majimbo huenda yakafanya hivyo kabla ya wakati huo.

Alipoulizwa kuhusu hatari ya taifa hilo kuondoa marufuku ya kutoka nje mapema, Rais Trump alisema: "Kuna hatari ya vifo ikiwa wataendelea na amri hiyo."

Mamilioni ya Wamarekani wamepoteza kazi kutokana na amri iliyowekwa ya kudhibiti maambukizi ya corona kote nchini huku viwango vya ukosefu wa ajira vikivunja rekodi.

Mauzo ya bidhaa yameshuka kwa asilimia 8.7 mwezi Machi, kiwango ambacho hakijawahi kushuhudiwa tangu mwaka 1992, kwa mujibu wa ripoti ya serikali iliyotolewa siku ya Jumatano.

Magavana katika majimbo ya Connecticut, Maryland, New York na Pennsylvania wametoa amri au muongozo wa wakazi kuvalia barakoa wanapojiandaa kurejelea shughuli zao za kawaida katika jamii wiki chache zijazo.

Siku ya Jumatano, Meya wa Los Angeles, Eric Garcetti, alisema mikusanyiko mikubwa ya watu kama vile ya michezo na matamasha huenda isiruhusiwe katika jiji hilo hadi 2021.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, alisema China lazima iweke wazi suala la virusi vya corona, alipompigia mwenzake wa Beijing, Yang Jiechi.

Pompeo alikuwa akilaumu Beijing kwa kuficha kiwango cha mlipuko wa virusi vya corona siku za awali, madai ambayo China inapinga.

**BBC**

# Rais atangaza kuwaachia wafungwa kisa corona

**YAOUNDE,** Cameroon

RAIS wa Cameroon, Paul Biya, ametangaza kuachiliwa huru kwa wafungwa ambao hakutaja idadi, hatua ambayo inatarajiwa kuanza kutekelezwa.

Hatua hiyo imekuja katika muktadha uliowekwa katika siku za hivi karibuni, baada ya baadhi ya mashirika ya kiraia na vyama vya siasa kutoa wito wa kuwaachilia huru wafungwa ambao wanakabiliwa na hatari ya maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona.

Hata hivyo, idadi ya wafungwa wanaotarajiwa kuachiliwa huru haijajulikana. Agizo la Rais Biya, lililosomwa kwenye redio ya taifa lakini halikutaja idadi ya watu watakaoachiwa huru.

Hata hivyo, tangazo hilo limebaini kwamba wafungwa waliopatikana na hatia ya ufisadi, ubadhirifu au ugaidi, agizo hilo haliwahusu.

Kwa hivyo, wafungwa wanaoitwa wa kifahari, waliofungwa katika muktadha wa mapambano dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma, agizo hilo halitawahusu. Vilevile, tangazo hilo halitawahusu watuhumiwa waliopatikana na hatia katika machafuko yaliyotokea katika maeneo wanakozungumza Kiingereza na ambao kwa sehemu kubwa walikata rufaa dhidi ya hukumu yao.

Wakili Alice Nkom alisema amefurahishwa na agizo hilo, kwani asilimia 70 ya wafungwa katika magereza ya Cameroon agizo hilo haliwahusu.

Kutokana na agizo hilo watu kati ya 2000 hadi 3000 wataachiliwa huru, kwa mujibu wa Maximilienne Ngo Mbe kutoka shirikisho la wanaharakati wa haki za binadamu katika ukanda wa Afrika ya Kati.

**RFI**

# Nchi masikini zasamehewa madeni

**WASHINGTON,** Marekani

WAKUU wa nchi 20 zenye nguvu kiuchumi na zinazoinukia kiuchumi duniani (G20), wamekubaliana kusamehe kwa muda madeni ya nchi masikini duniani.

Mawaziri wa fedha na magavana wa benki kuu wa G20 wamesema wanaunga mkono kusimamisha kwa muda malipo ya madeni kwa nchi hizo ambazo zinahitaji kuvumiliwa.


Uamuzi huo umefikiwa jana katika mkutano wao uliofanyika kwa njia ya video.

Muda huo unaanza Mei Mosi hadi mwishoni mwa mwaka 2020 na deni kuu pamoja na malipo yote ya riba yatasimamishwa.

Mkurugenzi wa Shirika la Fedha Duniani (IMF), Kristalina Georgieva, aliupongeza uamuzi huo.

Katika taarifa yao ya pamoja IMF na Benki ya Dunia zimesema zimefurahishwa na hatua hiyo ya G20 ya kuitikia wito wao wa kiziruhusu nchi masikini duniani ambazo ziliomba kuvumiliwa na kusimamishwa kwa muda ulipaji rasmi wa madeni yao kuanzia tarehe moja ya mwezi Mei

**DW**



# Moura ataka Kane abaki Spurs

**LONDON,** England

LUCAS Moura ana matumaini Harry Kane atabakia Tottenham, akikubali kwamba itakuwa ni vigumu kumpata mshambuliaji mwingine wa kuziba nafasi yake.

Kane amekuwa akihusishwa kuondoka hapo Spurs na mwezi uliopita alinukuliwa akisema "atabakia hapo itakapobidi tu".

Lucas amesema Kane, ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda Real Madrid, ni mtu muhimu kwa Tottenham na anataka mshambuliaji huyo wa timu ya taifa ya England kubakia kwa klabu hiyo ya Ligi Kuu England.

"Ni vigumu kuzungumza kuhusu majaliwa yake, kuhusu makubaliano yake kwa sababu ni uamuzi wa mtu binafsi.

"Nina uhakika kila msimu Tottenham inapata ofa kwa ajili ya kumuuza Harry Kane," amesema akiiambia Sky Sports.

"Sio mimi ninayeamua, lakini bila shaka nataka kucheza naye msimu ujao. Nataka abakie na sisi kwa sababu ni mchezaji muhimu mno kwetu na sio rahisi kumpata kama yeye.

"Kila mmoja anajua kwamba ni mchezaji mkubwa. Ni mchezaji muhimu sana kwetu, ni mshambuliaji wetu na anafunga mabao karibia katika kila mchezo.

"Nina uhakika Jose Mourinho anataka kumbakiza. Anamhesabia yeye kwa msimu wote na kumtegemea."



# Luiz asifia mchango wa Arteta

**LONDON,** England

DAVID Luiz amemsifia mchango wa Mikel Arteta tangu achukue nafasi ya kuinoa Arsenal, akisema kocha huyo ameiweka klabu hiyo pamoja.

Arteta alichukua nafasi ya kuinoa klabu hiyo Desemba mwaka jana, akishinda mechi nane na kupoteza mbili kwenye michezo 16.

David Luiz amesema nahodha huyo wa zamani wa Arsenal amemfanya aielewe vizuri klabu na kuwaleta watu wote pamoja.

"Kitu hiki kimenifurahisha tangu siku ya kwanza alipowasili, ameileta klabu yote pamoja, sio wachezaji tu," amesema mlinzi huyo akiiambia ESPN Brasil Jumatano.

"Na ningependa klabu iendelea kuwa pamoja, kwa mawazo yaleyale, na malengo yake yote mazuri.

"Kila mmoja anaelewa kwanini tupo hapa, nani aliyekuwa anatuwakilisha na nini tunachotakiwa kukifanya."



# Madrid yawania kumsajili Aubameyang

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imemfanya Pierre-Emerick Aubameyang 'kipaumbele kikubwa' kipindi cha usajili wa majira ya joto na wanawania kumsajili mshambuliaji huyo wa Arsenal.

Miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, wamekuwa wakipambana kuimarisha safu yao ya ushambuliaji tangu kuondoka kwa Cristiano Ronaldo hapo Bernabeu na kwenda Juventus mwaka 2018.

Hata hivyo, Zinedine Zidane anaamini Aubameyang anaweza kuliziba vizuri pengo hilo huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon akiwa bado hajakubali kuongeza mkataba pale kwenye uwanja wa Emirates.

Kwa mujibu wa gazeti la Sport la nchini Hispania, mshambuliaji huyo 'ameomba kuondoka kipindi cha majira ya joto' na klabu kadhaa zimekuwa zikimuwania kwa miezi ya hivi karibuni ikiwemo Barcelona, Inter Milan, Manchester United na Paris Saint-Germain.

Aubameyang amebakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa sasa na Madrid wanaamini wanaweza kumsajili mshambuliaji huyo kwa ada ya pauni milioni 44.

Tangu ajiunge na Arsenal, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 amefunga mabao 61 katika mechi 97 alizocheza.

Lakini kwakuwa washikabunduki hao wana nafasi ndogo ya kufuzu kucheza Ligi ya mabingwa msimu ujao majaliwa ya mshambuliaji huyo yapo shakani katika kikosi hicho cha kocha, Mikel Arteta.

Zidane ameamua kumgeukia Aubameyang kwa sababu anaona kuna uwezekano mdogo wa kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez ambaye pia anawaniwa na Barcelona.

## HABARI MICHEZO

# AC Milan yakataa kumsajili Lallana




**MILAN,** Italia

AC Milan imepiga chini nafasi ya kumsajili kiungo wa Liverpool, Adam Lallana, kwa mujibu wa gazeti Daily Mail.

Rossoneri imekuwa ikijipanga kukijenga kikosi chake wakati wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja na tovuti ya Calciomercato.com imedai kuwa Lallana amepewa ofa na miamba hao wa Serie A.

Hata hivyo, Milan haioni kama mchezaji huyo ni chaguo lao na kwamba hawezi kuongeza nguvu kwenye kikosi chao.

Mkataba wa Lallana pale Liverpool unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa Juni mwaka huu na atakuwa amemaliza kipindi cha miaka sita aliyokaa na klabu hiyo ya pale Merseyside.

Kocha wa wekundu hao, Jurgen Klopp alimtaka Lallana asaini kuongeza mwaka mmoja, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 hakuonekana kuitaka ofa hiyo na hivyo anaweza kuwa huru mwishoni mwa msimu.

Akizungumza Novemba mwaka jana, Klopp alisema: "Sijui nini kitatokea Mei kwa mtu yoyote, lakini kama mtu akipata nafasi ya kucheza anatakiwa kujituma. Na hicho ndio anachofanya Adam."

Lallana amefunga mabao 22 na kutoa asisti 22 katika mechi 178 alizoichezea Liverpool tangu alipotua hapo kwa pauni milioni 25 akitokea Southampton Julai mwaka 2014.

Kwa nyongeza, amefunga mabao matatu katika mechi 34 alizoichezea timu ya Taifa ya England tangu alipoanza kwa mara ya kwanza kwenye mchezo wa kirafiki wa kipigo cha 2-0 dhidi ya Chile Novemba mwaka 2013.

## Bruno: Watu wamesahau ubora wa Pogba

**MANCHESTER,** England

BRUNO Fernandes anaamini shutuma dhidi ya Paul Pogba zimesahaulisha kipaji cha mshindi huyo wa Kombe la Dunia na anasubiria kwa hamu kucheza nae pale Manchester United.

Pogba mara kwa mara amejikuta akijiweka kwenye matatizo yeye mwenyewe tangu aliporudi pale Old Trafford kwa ada ya rekodi ya pauni milioni 90 kutoka Juventus Agosti mwaka 2016.

Mchambuzi wa Sky Sports na nahodha wa zamani wa Liverpool, Graeme Souness mara kwa mara amekuwa akimshutumu mchezaji huyo na mapema wiki hii alishambuliana kwa maneno na Pogba.

Lakini Fernandes, ambaye amekuwa na mwanzo mzuri tangu kutua hapo United akitokea Sporting CP Januari mwaka huu, anafikiri Pogba atanufaika na imani ya kuimarika kwa mashetani wekundu hao wakati ligi itakapoanza tena baada ya kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.




"Nasubiria kwa hamu kucheza pamoja nae. Nafikiri tuna wachezaji wengi kwenye nafasi ya kiungo," amesema Fernandes wakati wa mahojiano ya maswajili na majibu kwenye tovuti ya United kuhusu Pogba, ambaye hajacheza tangu Desemba mwaka jana baada ya kuumia kifundo cha mguu.

"Paul ameumia kwa muda mrefu, na tutajua ubora wake wakati ligi itakapoanza tena.

"Tunaweza kusema kwenye soka mara nyingi watu wanasahau namna gani ulivyo bora wakati unapofanya makosa.

"Unaweza kufanya vizuri kwa mechi 34, na mchezo mmoja ukafanya vibaya na kila mmoja atakumbuka hilo tu."

# United yaamua 'kumtosa' Chiesa

**MANCHESTER,** England




MANCHESTER United imeamua kughairi uamuzi wake wa kuwania saini ya Federico Chiesa baada ya klabu yake ya Fiorentina kusisitiza kumetokea mabadiliko ambayo yamesababisha nyota huyo kuwa na furaha ya kubakia Florence.

Kocha Ole Gunnar Solskjaer alikuwa ameridhishwa na kiwango cha winga huyo ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 60, tangu mapema Februari mwaka huu.

Mashetani Wekundu walivutiwa na kiwango cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ambaye ni mtoto wa straika wa zamani wa Serie A na Timu ya Taifa ya Italia Enrico.

Winga huyo amefunga mabao saba katika mechi 26 alizocheza na kutoa pasi tano za mwisho.

Lakini Rais wa Fiorentina, Rocco Commisso tayari ameshatoa onyo kwa United kuacha kumfuatilia winga huyo.

"Napenda kuwekam wazi kuwa ninahitaji kuwa na wachezaji ambao wanataka kubakia hapa," alimwambia mtangazaji wa Top Calcio 24.

"Nimembakiza [Chiesa] msimu huu, lakini kwa sababu anataka kubakia hapa na tutajaribu kufanya kila kinachowezekana kumfanya awe na furaha.

Juventus imetajwa pia kumwania Chiesa ambaye ana mkataba na klabu yake hadi ifikapo mwaka 2022.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI KUSTAAFIA SOKA BARCELONA

**Ni kutokana na uamuzi wa kusaini mkataba mwingine mpya na klabu hiyo, huku Neymar...**

**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI nyota wa Barcelona, Lionel Messi, anatarajiwa kusaini mkataba mpya wa kuitumikia klabu hiyo huku mchakato wa Neymar kujiunga na timu hiyo ukionekana utafanikiwa, taarifa kutoka kwa Makamu wa Rais wa zamani wa Nou Camp, Emili Rousaud amesema.

Rousaud, pamoja na maofisa wengine watano walitangaza kujiuzulu katika bodi ya wakurugenzi wa timu hiyo wakipinga namna Rais Josep Maria Bartomeu anavyoiendesha klabu hiyo.

Lakini kwa sasa ameamua kuzungumzia hatima ya Messi sambamba na mchakato wa kurejea kwa mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Neymar.

**Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina utakamalizika ifikapo majira ya joto mwakani na tayari alianza kuhusishwa na kujiunga na Inter Milan.**

"Nafikiri Messi na Barcelona watafikia katika makubaliano kuhusiana na kuongeza mkataba mpya," Rousaud aliiambia ESPN Deportes.

Kocha Quique Setien amesema sasa majaliwa ya Messi hayapo kwenye shaka kubwa kutokana na awali kuwa na mgogoro wa chini chini wa viongozi hapo Camp Nou.

Licha ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kusimamishwa kutokana na mlipuko wa corona, Barcelona imeendelea kuwa na mgogoro unaofukuta kwa wiki kadhaa ndani ya viongozi wa klabu hiyo.

Katika taarifa yake, Rousaud aliwashutumu baadhi ya viongozi ndani ya Barca bila kuwataja majina kwamba wanahusika na rushwa.

Messi mwenyewe aliingia kwenye vita ya maneno na Mkurugenzi wa michezo, Eric Abidal, ambaye aliwashutumu baadhi ya wachezaji kutojituma na kusababisha kocha Ernesto Valverde kutimuliwa.

Licha ya kuhusishwa na mpango wa kutakiwa na Manchester City na Inter Milan lakini Setien anajiamini kwamba nahodha huyo atabakia kwenye kikosi hicho.

"Haya ni mambo ya kawaida kwa klabu kubwa kama hii," alisema akiiambia televisheni ya TV3. "Pengine kitu cha huzuni ni kwamba matatizo haya yanapelekwa hadi kwenye vyombo vya habari.

"Sidhani kama itatokea kumwachia kirahisi mchezaji kama Messi. Nina uhakika atabakia hapa na kumalizia soka lake kwenye dimba la Camp Nou."

## KWA UFUPI

### SANE AKARIBIA BAYERN

WINGA wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Leroy Sane (24), anakaribia kukamilisha mchakato wa kujiunga na Bayern Munich kwa ada ya pauni milioni 70. (Mirror)

### HATIMA EPL LEO

KLABU zinazoshiriki Ligi Kuu England zinatarajia kukutana leo ili kujadili uwezekano wa kuendelea na ligi hiyo ifikapo Juni 30, mwaka huu. Kama suala hilo litafikia katika kupiga kura, klabu 14 kati ya 20 zitakubaliana na uamuzi huo. (Guardian)

### BARCA YAMTAKA KANTE

BARCELONA inataka kumsajili kiungo wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ufaransa, N'Golo Kante (29). The Blues wanatarajia kushauri ili kukamilisha usajili huo, wabadilishane na winga Mbrazil Philippe Coutinho (27), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Bayern Munich akitokea Catalan. (Mundo Deportivo - in Spanish)

### ROMAGNOLI ATAJWA CHELSEA

CHELSEA imeweka wazi nia yake ya kumsajili nahodha na beki wa kati wa AC Milan na Timu ya Taifa ya Italia, Alessio Romagnoli, ambaye ana umri wa miaka 25. (Calciomercato - in Italian)

### HAVERTZ ANUKIA EPL

KIUNGO wa Bayer Leverkusen na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Kai Havertz (20), amesema kwa sasa yuko huru kuhama, Liverpool ni moja ya timu za Ligi Kuu England zilizoweka wazi nia ya kuwania saini ya nyota huyo. (Sport Bild - in German)

### GIROUD AJIONGEZA

STRAIKA wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud (33), amesema yuko tayari kukatwa sehemu ya mshahara wake ili kuhakikisha anabakia katika klabu ya Inter Milan majira ya joto. (Gazzetta dello Sport - in Italian)

### ROJO ANOGEWA ARGENTINA

BEKI Marcos Rojo ameiangukia Manchester United ili kumruhusu aendelee na mkataba wake wa mkopo katika klabu ya Estudiantes iliyoko Argentina, ambayo alitua Januari mwaka huu na kuonyesha kiwango kizuri. (Mail)

### LALLANA MAMBO BADO

VIGOGO wa Italia, AC Milan imeamua kusitisha nia ya kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Adam Lallana, katika majira ya joto. Nyota huyo wa zamani wa Southampton (31), anatarajiwa kumaliza mkataba wake Liverpool ifikapo Juni, mwaka huu. (Mirror)

### LACAZETTE HAKIJAELEWEKA

ARSENAL inatarajia kumweka sokono straika Mfaransa Alexandre Lacazette mwishoni mwa msimu huu, huku Atletico Madrid ikitajwa inamwinda nyota huyo mwenye umri wa miaka 28. (AS - in Spanish)

### AUBAMEYANG NJIA NYEUPE

MABOSI wa Arsenal wamesema wameshakubali kumpoteza straika wake raia wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang (30), ambaye anatakiwa na Real Madrid. Zinedine Zidane pia anatajwa kumwinda mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez (Sport- in Spanis).

### MARTINEZ AIOTA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Lautaro Martinez, amesema kuwa anataka kuona mchakato wa kuondoka katika klabu hiyo ya Italia na kujiunga na Barcelona unakamilika. (Sport - in Spanish)

# HATIMA YA NGOMA AZAM FC HAIJULIKANI

**Na Adam Fungamwango**

HATIMA ya mshambuliaji wa mabingwa watetezi wa mashindano ya Kombe la FA, Azam FC, Donald Ngoma, ndani ya kikosi hicho iko mikononi mwa Kocha Mkuu, Aristica Cioaba, imeelezwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat', amesema mkataba wa straika huyo wa zamani wa FC Platinum na Yanga unaelekea ukingoni, lakini suala lake la kubaki au kuondoka liko chini ya mikono ya Cioaba.

"Ni kweli, lakini kwa sasa ligi imesimama, ingekuwa inaendelea ndiyo tungepata tathmini kutoka kwa kocha juu ya kiwango cha Ngoma na wachezaji wengine ambao mikataba yao inaelekea ukingoni, lakini kutokana na janga hili la Corona kila kitu kimesimama hakuna kitu kinachoendelea," alisema Popat.

Alisema kama ligi ingekuwa inaendelea, basi saa hizi wangekuwa wameshapata majina ya wachezaji ambao wataendelea nao na wale ambao hawataendelea nao.

"Nadhani tuvute subira ili tuangalie kama ligi itaendelea au haitoendelea, nadhani baada ya hapo ndipo tutapata tathmini kwa kocha kama tuendelee naye ama tusiendelee naye," alisema.

Hata hivyo alimsifu mshambuliaji huyo na kusema ni mchezaji mzuri na hata alipojiunga nao msimu uliopita wengi hawakutarajia kama angefanya vema, baada ya kutocheza kwenye mechi kadhaa za mwanzo wa ligi, lakini akafunga magoli mengi.

"Kwetu sisi ni mchezaji mzuri, lakini uamuzi tunamwachia kocha ndiye mwenye hilo jukumu, kwa sababu anayetaka kuendelea naye ndiyo kama unavyoona kuna baadhi ya wachezaji tumewaongeza mikataba, lakini suala la Ngoma bado," alisema kiongozi huyo.

Azam ilimsajili Ngoma akitokea Yanga, ambao aliwafungia magoli 27 kwa misimu mitatu aliyodumu.



Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), Nicholas Musonye (kushoto), akikabidhi nyaraka za baraza hilo kwa mrithi wake, Auko Gecheo. Katikati ni Rais wa Cecafa, Wallace Karia. **PICHA: MAKTABA**

# M-Bet yazindua ubashiri mpya

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI M-Bet, imezindua michezo ya kubashiri inayojulikana kama Simulated Reality League (SRL), kupitia Kampuni ya SportRadar, inayotoa huduma za teknolojia mbalimbali za michezo hiyo, imeelezwa.

SRL ni ingizo jipya katika orodha ndefu ya michezo inayoendeshwa na M-bet ikiwa ni aina ya ligi mpya inayojumuisha ubashiri wa kabla ya mechi na wakati mechi inaendelea, kwa kutumia teknolojia mpya ya ubashiri.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa M-Bet Group, Daniel Fischer alisema uwepo wa SRL na michezo mengine ya aina hiyo, inatoa fursa kwa M-bet kuendelea kutoa huduma kwa wateja wake walioko katika mataifa mbalimbali duniani.

Fischer alisema wateja wanaweza kushiriki kubashiri kabla ya mechi au wakati mechi zinaendelea katika ligi zao pendwa na teknolojia ya Sportradar inatoa mwanga na namna ya kuweza kuendelea kuwapa burudani wateja wake.

"Michezo hii kwa sasa inahusisha ligi kubwa kutoka nchini Uingereza, Ujerumani, Italia, Hispania na ligi nyingine za bara la Ulaya, kila mechi ni dakika 90 na unaweza kubashiri kwa timu uipendayo, kuangalia takwimu za mechi, msimamo wa ligi pamoja na kufuatilia ubashiri wako kupitia Live in play tracker (mubashara)," alisema.

Aliongeza uwapo wa SRL unatoa fursa kwa mashabiki wa ligi za soka za barani Ulaya kumalizia msimu kama ilivyokusudiwa huku mechi zote zikichezwa kama ratiba ya ligi ilivyopangwa.

## Mwadui yafikiria 'Top 10' Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

HUKU hatima ya kuendelea au kutoendelea kwa mechi za Ligi Kuu Bara msimu mwaka 2019/20 ikiwa haijafahamika, uongozi wa Mwadui FC umesema malengo yao ni kuona wanamaliza kwenye nafasi 10 za juu katika msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Mwadui FC, Ramadhani Kilao, alisema licha ya kutojua hatima ya ligi, lakini mipango yao ni kuhakikisha wanamaliza katika nafasi nzuri na hatimaye kujiepusha na janga la kushuka daraja.

Kilao alisema kwa sasa 'wanaumiza kichwa' kuhakikisha watakaporejea katika ligi, timu yao itafanya vizuri na kufikia mipango hiyo waliyojiwekea.

"Tupo katika nafasi ya 12 katika msimamo, hapa tulipo sio salama kwetu, tunaendelea kusisitiza benchi la ufundi kuwafatilia wachezaji wetu kwa ukaribu hasa kipindi hichi cha janga la Corona," alisema Kilao.

Aliongeza wanawakumbusha wachezaji wao kuzingatia programu za mazoezi walizopewa katika kipindi hiki ili ligi itakaporejea tena wawe kwenye kiwango bora na kitakachokabiliana na ushindani.

Mwadui FC ambayo imecheza mechi 28, ina pointi 34 wakati vinara wa ligi hiyo ni Simba yenye pointi 71.

## Kipa Zimamoto FC afariki dunia

**Na Hawa Abdallah,** Zanzibar

ALIYEKUWA golikipa wa Zimamoto FC inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, Khamis Uzid Omar, amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mrefu na kuzikwa jana kwenye makaburi ya Upenja Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Zimamoto, Ally Jongo, alisema marehemu Omar alikuwa anasumbuliwa na maradhi ya kupooza kwa muda mrefu ambayo yalisababisha kushindwa kuitumikia timu yake katika msimu huu.

Jongo alisema Zimamoto itaendelea kumkumbuka mlinda mlango huyo kutokana na mchango wake alioutoa katika timu hiyo iliyowahi kupeperusha vema bendera ya Zanzibar katika mashindano mbalimbali.

"Timu yetu imepata pigo, na pengo ambalo litachukua muda kusahaulika, alikuwa mchezaji hodari sana na mwenye mafanikio katika soka la Zanzibar na timu yetu kwa ujumla, lakini ni hatima siku yake ilifika na Allah akamchukua kiumbe chake, hatuna budi kushukuru," alisema.

# Michezo

Ijumaa Aprili 17, 2020

Nipashe


## Messi kustaafia soka Barcelona




HABARI UK.22



Straika wa Tottenham na Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, ameweka wazi hahofii kuondoka Spurs na uhamisho wake wa pauni milioni 200 kuelekea Manchester United unatarajiwa kuweka rekodi ya dunia. **PICHA: MTANDAO PICHA: MTANDAO**.

# LIGI KUU BARA BADO SHAKANI

## ●●● TFF yafunguka kufanya vikao vya mara kwa mara na serikali ili kujadili hatima ya...

**Na Somoe Ng'itu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesema hatima ya kuendelea kwa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa mwaka 2019/20 bado haijajulikana kutokana tamko jipya lililotolewa na serikali la kusimamisha michezo kwa muda usiojulikana.

Mapema wiki hii, serikali ilitoa tamko la kutoruhusu mikusanyiko ikiwamo Ligi Kuu Bara, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili na mashindano mengine mbalimbali ili kuendelea kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19).

Awali TFF ilisema endapo hali ya maambukizi itakuwa haijaimarika, Ligi Kuu Bara inaweza kurejea, lakini itachezwa bila ya mashabiki, uamuzi ambao ulionekana kupingwa na baadhi ya timu.

Akizungumza na Nipashe, kiongozi mmoja wa juu wa TFF (jina tunalihifadhi), alisema shirikisho hili liko katika mazungumzo na viongozi wa serikali kuhusiana na tathmini iliyopo ya ugonjwa huo ambao umesimamisha pia ligi mbalimbali duniani.

**Kiongozi huyo alisema kuwa bado hakuna uamuzi mpya uliochukuliwa mpaka jana na hii inalenga kuweka mbele maslahi ya afya za wadau wake.**

"Bado tunayafanyia kazi kwa kuangalia hali iliyopo, tunashukuru tunafanya kazi kwa karibu na serikali, mamlaka za nchi," alisema kwa kifupi kiongozi huyo.

Alisema bado hakuna maoni au mapendekezo yoyote yaliyowasilishwa na klabu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kuhusiana na nini kifanyike ili kumaliza msimu huu.

"Hapana, hakuna klabu yoyote iliyowasilisha maoni," aliongeza kiongozi huyo.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, aliliambia gazeti hili wao wanaamini ligi hiyo itamalizika na bingwa atapatikana baada ya kila timu kukamilisha idadi ya mechi 38 zinazotakiwa.

"Ninavyofahamu mimi kipindi hiki ligi ilikuwa inasimama hadi Aprili 28, mwaka huu kwa sababu Timu ya Taifa (Taifa Stars), ingekuwa kwenye fainali za CHAN, hakijaharibika kitu, ikimalizika bingwa sie, ikisimama bingwa sie," Manara alisema.

Simba yenye pointi 71 ndio mabingwa watetezi na vinara wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 20 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

## Simba, Yanga zachambuliwa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar ya Manungu, Turiani mkoani Morogoro, Zuberi Katwila, amesema timu yake itasajili kwa kishindo wachezaji kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Bara baada ya vigogo wa soka nchini, Simba, Yanga na Azam FC kumaliza 'kukibomoa' kikosi chake.

Katwila ameliambia gazeti hili kwa sasa yupo kimya kwa sababu bado hajakabidhi ripoti ya kiufundi kwa uongozi wa klabu hiyo kutokana na kuamini baadhi ya nyota wake wataondoka na kujiunga na timu nyingine.

Katwila alisema anasubiri kuona nafasi ambazo zitakuwa wazi ili kuziba mapengo na hiyo hutokea kila msimu unapomalizika.

"Wasione Mtibwa tumekaa kimya katika usajili, ukimya huu unakishindo mbele, kikubwa tunasubiri hizi timu kubwa (Simba, Yanga na Azam), kufanya usajili wao, nina imani kwetu kila msimu anaondoka mtu, sasa huo muda utakuwa mzuri kwangu kuziba nafasi ya aliyeondoka," alisema Katwila.

Kocha huyo alisema hawezi kuweka wazi nafasi atakazoziimarisha kwa sababu anahitaji kusubiri sura halisi ya wachezaji watakaobakia kutokana na uzoefu aliokuwa nao.

"Hapa ni chuo, hivyo tusiposajili kutoka nje basi tuna wachezaji tutakaowapandisha kutoka katika kikosi cha vijana, watakuja kufanya vizuri kwa kusaidia timu yetu kama ilivyokuwa kwa wengine hapa," alisema Katwila.

Hata hivyo Mtibwa Sugar inayoundwa na wachezaji wazawa pekee, msimu huu imekuwa na matokeo ya kusuasua.

Baadhi ya wachezaji wa Mtibwa Sugar ambao waliondoka na wanang'ara katika timu hizo za jijini Dar es Salaam ni pamoja na Hassan Dilunga, Muzamiru Yassin, Shiza Kichuya walioko Simba na Mudathir Yahya wa Azam FC.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >